# Kuchaguo Bibi-arusi
Los Angeles, California USA
Aprili 29, 1965J

1 Wagonjwa wengi sana. Siwezi kuwafikia wote kwa wakati mmoja. Lakini, sikilizeni.

Hakika nina furaha kuwa hapa tena, usiku huu, katika ukumbi huu mzuri, miongoni mwa kundi hili zuri la watu. Nasi tulikuwa tukiingia, huko nje, dakika chache zilizopita, watu waliosimama barabarani walisema wasingeweza kuingia. Nami nikasema, "Vema, labda naweza kuwatafutia nafasi." Nao wasingewaruhusu waje. Kwa hiyo nasikitika hatuna nafasi ya kutosha kwa ajili yao. Walisema orofa ya chini ilikuwa imejaa, pia. Na kwa hiyo tunasikitika juu ya jambo hilo. Lakini tuna furaha kuwa hapa, na tuna furaha kuona kundi hili lote zuri la wahudumu, wafanyabiashara hapa, na ninyi nyote wajumbe kutoka sehemu mbalimbali nchini.

2 Nilikuwa na majaliwa makuu ya kuzungumza asubuhi ya leo kwenye kiamshakinywa, ambalo kwa kweli nathamini kuwa ni heshima kuzungumza mbele ya watu wazuri kama hao. Nilikuwa kwenye somo la: *Kapi Halitarithi Pamoja Na Ngano*. Sikuweza kulimaliza. Na halikuwa kosa la yu—yule ndugu. Alijaribu kuwashawishi wasimamizi waturuhusu tukae kwa muda kidogo zaidi, bali hakuweza kufanya hivyo. Hakika nathamini jambo hilo, Ndugu Demos. Hilo ni zuri, zuri sana. Hakika nawashukuru kwa wema wenu, kila mmoja. Lakini hawangeturuhusu tufanye hivyo. Kwa hiyo ilitulazimu tu ku—ilitulazimu kufunga. Nitachukua jambo hilo, wakati mwingine, kumalizia huo: *Kapi Halitarithi Pamoja Na Ngano*. Je! Mluelewa huo, ninyi mliokuwa hapa? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Ninatumaini kulikuwa na ya kutosha kuufanya ueleweke.

3 Sasa, ninajua, usiku wa leo, kuna jopo, pia, kwa hiyo sitaki kuwaweka hapa muda mrefu vya kutosha mpate kukosa jambo hilo. Kwa sababu, nafikiri huo hakika ulikuwa muhimu sana kwa—kwa waaminio Wapentekoste, ule mjadala tuliouona hivi majuzi usiku. Kundi zuri sana la watu, majibu mazuri sana, ya wazi. Ilinifanya nijisikie vizuri sana, kuuona huo. Ninatumaini ya kwamba Bwana ataubariki, usiku huu. Na yeyote yule anayeutazama, na waamini. Hayo yangekuwa ndiyo maombi yangu manyofu.

4 Na ripoti nyingi sana zikija, leo, kutoka kwenye barua na kwa simu, za watu wengi sana wanaoponywa katika mkutano huu. Nilifurahi hayo sana. Hiyo, hiyo ni, kuwaona watu wagonjwa, kwa namna fulani hiyo ndiyo huduma yangu.

Na—napanda hapa juu kuhubiri. Mimi, mnajua, mimi si mhubiri. Lakini mimi, nikiwa na hii, sarufi yangu ya Kentucky, "yake, haiko'" na—na maneno hayo yote, hivyo si—siwezi kusema kama mtu aitwaye mhubiri wa kisasa wa siku hizi. Ni—nisingeweza kupachukua mahali hapo, kwa sababu si—sina elimu.

Lakini napenda kuelezea yale ninayojua kuhusu Hilo, kwa wengine, ama yale ninayojisikia kwamba najua kuhusu Hilo, kwa wengine, jinsi nilivyojifunza Hilo, jinsi Yeye alivyo kwangu. Yeye ndiye maishani yangu yote, yote ambayo ningeweza kutarajia kuwa, na mengine mengi sana kuliko vile nilivyowahi kuwaza, kwamba ingekuwa vigumu kupata rafiki, ni vigumu, duniani, nilipokuwa mvulana mdogo. Lakini hakika nashukuru kwa ajili ya marafiki wakuu leo hii.

Mimi … [Ndugu fulani anasema, "Kuna shida kidogo kusikia huko nyuma, Ndugu Branham. Sogea karibu zaidi." — Mh.] Loo, samahani. Ki—kidogo niko kando hapa, mahali fulani, alisema.

5 Sasa, kuingia moja kwa moja kwenye ibada, hebu na tufungue kwa ajili ya kusoma Maandiko fulani. Mimi—mimi daima napenda kusoma Biblia, kwa sababu ni Neno la Mungu. Naamini hilo. Nami naamini Hilo ni Neno la Mungu lisilokosea. Na sasa nina Maandiko machache yaliyoandikwa hapa, na muhtasari ambao ningependa kuurejea, kwa dakika chache, labda kwa dakika arobaini na tano.

Na ndipo basi tutaondoka kwa wakati kwenda kuona jopo hili zuri tena usiku huu. Nami natumaini ya kwamba Mungu ataendelea kuwabariki moja kwa moja hadi mwisho. Nami najua yale mnayopaswa kufanya. Nami napaswa kuendesha gari hadi Tucson, hata hivyo, usiku wa leo, unaona, hivyo mnaweza kuwazia. Hiyo ni safari ya kuendesha gari masaa kumi.

Na naondoka kwenda ng'ambo, na sina budi kudungwa sindano ya homa ya manjano kwa majaribio asubuhi serikalini. Hivyo ni—sina budi kufika kule. Ilinipasa kuiahirisha, hivi majuzi, nao hawatakubali "la" kama jibu tena sasa. Na nimebakiza moja ya pepopunda na ya homa ya chawa, na ya kuniongezea nguvu.

6 Kwa hiyo, nashukuru sana kwa ajili ya nafasi hii, na—na mkutano huu mzuri tuliokuwa nao kabla ya hii mikutano. Hakika iliusisimua moyo wangu. Ninyi ni kundi zuri la watu. Natumaini ya kwamba Mungu atawabariki.

Wakati ile saa kuu ilipo … Yule mnyama mkubwa sana anayekaa kule, aliyejiviringisha kule Alaska, siku chache zilizopita, akalirusha mkia wake tena asubuhi hii, huko karibu, huko karibu na Washington. Angeweza kuelekea upande huu, kirahisi sana. Na kama Roho Mtakatifu akiniambia dhahiri …

Mtu fulani amekuwa akijibu … akiniuliza kwamba, "Je! Itatendeka hapa, Ndugu Branham?" La, sijui

hilo. Sijui tu, mpaka nijue. Huo ndio ukweli.

Daima nataka kuwa mwaminifu kwenu. Mimi sitadhania tu, kuchukua mawazo yo yote, ama mengine, yale ninayoamini, ama kitu kama hicho. Nitakapowaambia, itakuwa. Vema, itampasa Yeye aniambie, kwanza, na ndipo nitawaambia. Na—najua ulimwengu mzima uko katika hali ya kutetemeka. Tuko katika wakati wa mwisho. Lakini kitu kimoja ambacho nimejaribu kuwa …

7 Ndugu Shakarian alikuwa akisema asubuhi ya leo, jinsi alivyokuwa akipitia kwenye mistari ya maombi, na kufikia kule na kupata hizo kadi kabla watu hawajaja, na kuziangalia, na kuona kama—kama niliwaambia yale waliyokuwa wameandika mle. Wao huandika vitu vya kila namna kwenye kadi zao za maombi, mnajua, naye alitaka tu kuona kama ilikuwa ni kweli. Yeye alisema, kutoka kwa mamia ambazo alikuwa amechunguza, hakujawahi kuwa na kosa moja. [Ndugu Shakarian anasema, "Hapajakuwepo na kosa moja kamwe." — Mh.] Kamwe hakutakuwa na kosa moja, unaona, kwa sababu, mradi—mradi tu ni Mungu. Kama nikijiingiza mwenyewe ndani ya jambo hilo, basi ni kosa papo hapo kwanza.

Msichana mdogo ambaye baba yake ameketi, akinisikiliza sasa, alinijia, si muda mrefu uliopita. Alikuwa na ndoto. Akasema, "Ndugu Branham, ndoto hii ina maana gani?"

Nikasema, "Sijui, dada. Itanipasa kutafuta kujua, kama Bwana ataniambia." Hivyo nikaendelea na kujaribu kumwuliza Bwana, Naye hakuniambia kamwe.

Yule msichana mdogo akarudi tena. Akasema, "Vema, sasa iko wapi fasiri ya ndoto yangu?"

Nikasema, "Njoo hapa, mpenzi, uketi chini." Nikasema, "Baba yako na mama yako ni rafiki zangu wazuri sana. Unaona? Nao wamekuja kutokea mbali sana huko Canada, wamestaafu, na kukaa hapa pamoja nami. Wanaamini haya, yale ninayojaribu kusema. Na sijawahi kumwambia mtu ye yote jambo lisilo kweli, kwa kusudi, katika maisha yangu. Kama mimi … Nafikiri najua maana ya ndoto hiyo. Lakini mpaka niione ndoto hiyo mimi mwenyewe, na ndipo Yeye aniambie inamaanisha nini, siwezi kukuambia. Unaona, kama nikitengeneza tu kitu fulani, huenda kukawa na wakati ambapo utanihitaji kati ya uhai na mauti, na ndipo usingejua kama uniamini ama la."

8 Kama nikiwaambia jambo lo lote katika Jina la Bwana, hakika ni hivyo. Huyo Ndiye aliyeniambia jambo hilo. Na kufikia sasa, katika miaka hii yote, kote ulimwenguni, na ulimwenguni mwote, haijawahi kukosea hata wakati mmoja. Maana … Na, sasa, unajua mwanadamu hawezi kuwa asiyekosea hivyo. Inahitaji Roho wa Mungu kufanya hayo.

Na sasa nina Ujumbe ambao nawajibika nao. Na mara nyingi nimekuwa nikichukuliwa, miongoni mwa watu, vema, labda mtu ambaye hakuketi chini na kuwazia kidogo, ya kwamba nilikuwa m—a, loo, mtu mbaya sana, kwamba sikuwapenda watu, nami daima nilikuwa nikiwakatakata. Na sivyo ilivyo. Sivyo ilivyo. Nawapenda watu. Lakini, mnajua, upendo husahihisha.

9 Kama mvulana wako mdogo alikuwa ameketi barabarani huko, nawe ukasema, "Junior, mpenzi, sitaki wewe uwe huko, lakini …" Na magari yakipta kwa kasi karibu naye, nawe ukamleta ndani. Akakimbilia nje tena. Mbona, unapaswa kumsahihisha. Kama unampenda, utafanya jambo hilo. Huna budi kufanya hivyo.

Kama ukiona mtu akielea mtoni, kuelekea kwenye maporomoko ya maji, katika mtumbwi mdogo, na kwamba unajua kuwa huo mtumbwi unakwenda kuzama ufikapo kwenye maporomoko, je, ungesema, "Yohana, wewe, labda unapaswa kuwaza kidogo, labda hutafanikiwa?" Kama najua hatafanikiwa, nitamvuta nje ya huo mtumbwi, kama naweza, kwa sababu ni upendo unaofanya hivyo.

10 Na sasa, katika Jumbe hizi ninazonena, kamwe sijaribu kuingiza fundisho lo lote, ama mengineyo. Na—nafanya hayo katika kanisa langu mwenyewe. Lakini huko nje miongoni mwa wanaume na wanawake walio wa madhehebu tofauti na mawazo tofauti, najaribu tu kuzileta kwa urahisi, kuzielezea; lakini vya kunatosha kufikia mahali ambapo kama umezaliwa na Roho wa Mungu, naamini utaelewa ninalomaanisha, miongoni mwa Wakristo, Methodisti, Baptisti, Presbiteri, na wengineo.

11 Sasa, usiku huu, nataka kufungua Mwanzo, ile sura ya 24. Nataka kusoma ninii … kuanzia na ile aya ya 12 ya sura ya 24 ya Mwanzo.

> *Naye akasema, Ee BWANA Mungu … bwana wangu Abrahamu, nakuomba mambo yangu uyajalie yawe heri leo, ukamfadhili bwana wangu Abrahamu.*
>
> *Tazama, nimesimama hapa karibu na kisima cha maji; na binti za watu wa mjini wanatoka kuteka maji;*
>
> *Basi na iwe hivi; yule msichana nitakayemwambia, Tua mtungi wako, nakuomba, ninywe; Naye atasema, Unywe, nami nitawanywesha na ngamia zako pia; basi huyu na awe ndiye uliyemchagulia mtumishi wako Isaka; Na kwa hiyo nitajua* umenionyesha *fadhili... kwa bwana wangu.*

12 Na halafu katika Kitabu cha Ufunuo. Huo ni mwanzo wa Biblia, Mwanzo. Sasa, katika mwisho wa Biblia, nataka kusoma katika sura ya 21 ya Ufunuo, na ile aya ya 9.

Tunajua kile Maandiko haya ya Mwanzo hapa … Msome sura yote, mkitaka. Ni Mungu akimtuma Eliezeri. Ama, Abrahamu akimtuma Eliezeri, samahani, kumchagulia Isaka bibi-arusi. Ndipo yule Rebeka mrembo akaja, na katika jibu kamilifu kwa maombi ambayo—ambayo Eliezeri, mtumishi wa Abrahamu, alikuwa ndiyo tu ameomba.

Sasa katika ile aya ya 9 ya sura ya 21 ya Ufunuo.

> **Akaja mmoja wa wale malaika saba waliokuwa na vile vitasa saba vilivyojaa yale mapigo saba ya mwisho, naye akanena nami, akisema, Njoo huku, nami nitakuonyesha bibi-arusi, mke wa Mwana-Kondoo.*

13 Sasa nataka kuchukua kwa ajili ya somo, usiku huu, kwa ajili ya hilo: *Kuchagua Bibi-arusi.* Na hii ni, kama ndugu yangu anayerekodi hapa atapenda, hii ni kanda ambayo unaweza kuisambaza.

Na sasa, katika jambo hili, haimaanishi kabisa kwamba ninasema hili kwa kusanyiko hili lililopo hapa, bali hizi kanda huenda kote ulimwenguni. Zinafasiriwa katika, karibu, loo, lugha nyingi sana, hata katika nchi za makafiri kote ulimwenguni. Tunawatumia kanda, bure, kwenye chama cha kanisa. Na zinafasiriwa. Na kila mahali kote katika misitu ya Afrika, na India, na hizi kanda huenda kote ulimwenguni.

Sasa, kuchagua Bibi-arusi!

14 Katika mambo mengi ya maisha tumepewa uchaguzi. Njia ya maisha, yenyewe, ni uchaguzi. Tunayo haki ya kufanya njia yetu wenyewe, kuchagua njia yetu tunayotaka kuishi.

Elimu ni uchaguzi. Tunaweza kuchagua kama tutaelimishwa, ama kama hatutaelimishwa. Huo ni uchaguzi tulio nao.

Jema na baya ni uchaguzi. Kila mwanamume, kila mwanamke, mvulana na msichana, hana budi kuchagua kama watajaribu kuishi kwa usahihi ama kutoishi kwa usahihi. Ni uchaguzi.

Uchaguzi ni jambo kuu.

Kikomo chako wa Milele ni uchaguzi. Na labda, usiku huu, baadhi yenu mtafanya huo—huo uchaguzi, mahali ambapo mtaishi Umilele, kabla ibada hii haijaisha usiku huu. Kutakuwako na wakati mmoja, ambapo, kama ukimkataa Mungu mara nyingi, kutakuwako na wakati mmoja utakapomkataa mara ya mwisho. Kuna mstari kati ya rehema na hukumu. Na ni jambo la hatari kwa mwanamume ama mwanamke, mvulana ama msichana, kuvuka huo mstari, kwa kuwa hakuna kurudi wakati unapovuka mstari huo wa mwisho. Kwa hiyo, usiku huu, huenda ikawa ndio wakati ambapo wengi watafanya uamuzi wao—wao, pale ambapo wataishi Umilele isiyo na mwisho.

15 Kuna uchaguzi mwingine tulio nao maishani, huo ni, mwenzi wa maisha. Kijana mwanamume au kijana mwanamume, anayeingilia maisha, ame—amepewa haki ya kuchagua. Mvulana huchagua. Mwanamke kijana ana haki ya kuikubali ama kuikataa. Lakini bado ni uchaguzi, pande zote mbili. Wote wawili mwanamume na mwanamke, wanayo haki ya kuchagua.

Pia, unao uchaguzi, kama Mkristo.

Una uchaguzi wa kanisa, hapa Amerika, kufikia sasa, ambalo unaweza kwenda. Hayo ni majaliwa yako ya Kiamerika, kujichagulia kanisa lo lote unalotaka kuwa mshirika wake. Huo ni uchaguzi. Si lazima uhudhurie lolote la hayo, kama hutaki. Lakini kama unataka kubadilisha kutoka Methodisti kuingia Baptisti, au Katoliki kuingia Protestanti, au chochote kile, hakuna mtu anayeweza kukwambia ama kukufanya uhudhurie kwenye kanisa fulani. Huo ndio—ndio uhuru wetu. Hivyo ndiyo demokrasia yetu ilicho. Kila mtu anaweza kujichagulia mwenyewe. Uhuru wa dini, na hilo ni—ni jambo kuu. Mungu na atusaidie kulidumisha kadiri tuwezavyo.

16 Unao uchaguzi pia. Kama … Unapochagua kanisa hili, unaweza kuchagua kama wewe, katika kanisa hili, kama utachagua kanisa litakalokuongoza kwenye kikomo chako cha Milele. Unaweza kuchagua kanisa ambalo lina kanuni fulani ya imani, hata ukawaza kwamba kanuni hizo za imani ndizo kile unachokitaka hasa. Ama, kanisa lingine lililo na kanuni zao za imani.

Na kisha kuna Neno la Mungu, una uchaguzi kwake. Huna budi kufanya uchaguzi.

Kuna sheria isiyoandikwa miongoni mwetu, ya kuchagua.

Naamini ilikuwa ni Eliya, wakati mmoja, kule juu ya Mlima Karmeli, baada ya lile shindano la kuamua, katika saa kuu ya hatari sana ambayo tunakaribia sasa hivi. Labda, huenda ikawa kwako au kwangu, usiku huu, kwamba tufanye uchaguzi huu, kama lile tukio la Mlima Karmeli. Kusema kweli, nafikiri linaendelea, ulimwenguni kote, sasa. Lakini hivi karibuni kutakuwa na wakati ambapo itakulazimu kufanya

uchaguzi.

17 Na ninyi watu hapa, wa makanisa yenu ya kidhehebu, aminini tu hili, kwamba saa imewadia, mtakapochagua. Ama mtaingia kwenye Baraza la Ulimwengu, au hamtakuwa dhehebu tena. Itawabidi kufanya hivyo, na huo uchaguzi unakuja hivi karibuni.

Na ni jambo la hatari kungojea mpaka saa hiyo ya mwisho, pia, kwa sababu huenda ukachukua kitu ambacho kamwe usingeweza kujiondoa kwake. Unajua, kuna wakati ambapo unaweza kuonywa, kisha, kama ukivuka huo mstari wa onyo, basi tayari umetiwa alama upande ule mwingine, kupigwa chapa.

18 Kumbuka, wakati mwaka wa yubile ulipofika, na—na kuhani akaondoka akipiga baragumu yake, kwamba kila mtumwa angeweza kuwa huru. Lakini kama walikataa kukubali uhuru wao, ndipo ilimpasa apelekwe hekaluni, penye kizingiti, na kutobolewa sikio kwa uma, kisha akamtumikia bwana wake daima. Ilitiwa kwenye sikio lake kama mfano, wa kusikia. "Imani huja kwa kusikia." Yeye alisikia hiyo baragumu, bali hakutaka kuisikiliza.

Na mara nyingi, wanaume na wanawake husikia Kweli ya Mungu, na kuiona ikithibitishwa na kuhakikishwa, Kweli, lakini hata hivyo hawataki kuisikia. Kuna sababu nyingine. Kuna uchaguzi mwingine walio nao, kuliko kukabiliana na ile Kweli na kweli za mambo, kwa hiyo masikio yao yanaweza kufungwa yasisikie Injili. Hawataisikia tena kamwe. Ushauri wangu kwenu, Mungu anaponena na moyo wako, tenda mara moja wakati huo.

Eliya aliwapa uchaguzi, ambao wangepaswa kufanya: "Chagueni hivi leo mtakayemtumikia. Mungu akiwa ndiye Mungu, mtumikieni. Lakini ikiwa Baali ni Mungu, mtumikieni."

19 Sasa, tunapoona kwamba mambo yote ya kawaida ni mfano wa mambo ya kiroho, kama tulivyopitia katika somo letu asubuhi ya leo, kama jua na tabia zake. Hayo yalikuwa ndiyo Biblia yangu ya kwanza. Kabla sijawahi kusoma hata ukurasa mmoja katika Biblia, nilimjua Mungu. Kwa sababu, Biblia imeandikwa kila mahali katika maumbile, na yanalingana tu na Neno la Mungu: jinsi ambavyo kifo, kuzikwa, kufufuka kwa maumbile; na jua likichomoza, likipita, likitua, likifa, likichomoza tena. Kuna mambo mengi sana ambayo tungeweza kuyafananisha, Mungu katika maumbile, ambayo hatuna budi kuyaruka, kwa ajili ya Ujumbe huu.

20 Sasa, kama yale ya kiroho, au, yale ya kawaida ni mfano wa yale ya kiroho, basi, kuchaguwa bibi-arusi, katika yale ya kawaida, ni mfano wa kuchagua Bibi-arusi, yule Bibi-arusi, katika kiroho.

Sasa, ni jambo zito sana tunapoenda kuchagua mke, mwanamume, kwa kuwa nadhiri hapa ni mpaka kifo kitakapotutenganisha. Hivyo ndivyo tunavyopaswa kuidumisha. Nawe unaweka hiyo nadhiri mbele za Mungu, kwamba mauti pekee yatakayowatenganisha. Nami nafikiri tunapaswa … Mtu mwenye akili timamu, anayepanga maisha yake ya usoni, kwamba anapaswa kumchagua mke huyo kwa uangalifu sana. Uwe mwangalifu kwa yale unayofanya. Na mwanamke anayemchagua mume, ama anayekubali uchaguzi wa mume, anapaswa kuwa mwangalifu sana kwa yale anayofanya, na hasa katika siku hizi. Mwanamume anapaswa kuwaza na kuomba kabla hajamchagua mke.

21 Nafikiri, leo hii, iliyo na visa vingi sana vya talaka sasa, kwamba tunaongoza ulimwenguni huku Amerika, katika visa vya talaka. Tunaongoza ulimwengu wote. Kuna talaka nyingi hapa kuliko mahali pengine popote, taifa hili, na linasemekana kuwa, na kudhaniwa, kuwa taifa la Kikristo. Ni aibu jinsi gani, mahakama zetu za talaka! Nafikiri, sababu yake, ni kwa sababu wanaume wamemwacha Mungu, na wanawake wamemwacha Mungu.

Nasi tunaona, kwamba, kama mwanamume aliomba na mwanamke akaomba juu ya jambo hilo; si tu kuangalia macho marembo, ama mabega makubwa yenye nguvu, ama vitu kama hivyo, ama mapenzi mengine ya kilimwengu; bali angemtazama Mungu kwanza, na kusema, "Mungu, je! huu ndio mpango Wako?"

22 Nafikiri, leo hii, kuna udanganyifu mwingi sana, kama tu ilivyo shuleni. Wakati—wakati watoto wanapokuja, asubuhi, watoto wengi walio jirani, ambao—walio rafiki zangu, watakuja na kusema, "Ndugu Branham, je, utatuombea? Tuna—tuna mtihani leo. Ni—nilisoma usiku kucha, na sioni kama naweza—kama nimetosheka. Niombee." Nafikiri ya kwamba mtoto yeyote wa shule, kama ungeweza, kama … Na wazazi wakiwa mezani asubuhi: ungeweza kusema, "Mama, Yohana ana mtihani leo. Hebu tumwombee sasa." Nafikiri hilo lingeshinda yale yote ambayo ungeweza kufanya kwa njia nyingine yoyote, ama kuchungulia kwenye karatasi ya mtu mwingine na kudanganya. Nafikiri kama ungekuja tu na kuombea jambo hilo.

23 Na kama tungechunguza yale tunayofanya wakati tutakapoenda kuoana, tunapomchagua wake zetu, waume wetu, laiti tungeyachunguza kwa makini! Mwanamume anapaswa kuomba kwa bidii, kwa kuwa angeweza kuangamiza maisha yake yote. Kumbukeni, nadhiri ni "mpaka kifo kitakapotutenganisha," naye angeweza kuyaharibu maisha yake kwa kufanya uchaguzi mbaya. Lakini kama anajua ni nini, anachagua vibaya na anaoa mwanamke asiyefaa kuwa mke wake, naye anafanya hivyo haidhuru, basi ni kosa lake. Kama mwanamke akimchukua mume na anajua ya kwamba yeye hastahili kuwa mume wako, basi hilo ni

kosa lako mwenyewe, baada ya kujua yaliyo mema na mabaya. Hivyo, hupaswi kufanya hivyo mpaka uombe kwa bidii kabisa.

24 Vivyo hivyo katika kuchagua kanisa. Sasa, huna budi kuliombea kanisa unamoshiriki. Kumbuka, makanisa huwa na roho.

Sasa, sitaki kuwa mkosoaji. Lakini natambua kwamba mimi ni mzee, nami sina budi kuondoka hapa, mojawapo ya siku hizi. Na inanipasa kuwajibika kwenye Siku ya Hukumu kwa yale ninayosema usiku huu ama wakati mwingine wowote. Nami, kwa hiyo, sina budi kuwa mkweli kabisa na kushawishika kweli.

Lakini, unaingia kanisani, na kama utaangalia tabia ya hilo kanisa, hebu mwangalie tu mchungaji kwa muda kidogo, na mara nyingi utaona ya kwamba kanisa linatenda kama mchungaji wake. Wakati mwingine, nashangaa kama hatupati roho wa mwingine badala ya Roho Mtakatifu. Unafikia mahali ambapo mchungaji ni mtu wa mapinduzi kweli kwlei na kadhalika, utaona kusanyiko liko vivyo hivyo. Nitawaleta kwenye kanisa ambapo nimeona mchungaji akisimama, wakitikisa vichwa vyao huku na huko. Wewe liangalie kusanyiko, wanafanya jambo lile lile. Mchukue mchungaji, anayemeza tu kila kitu kwa pupa, kwa kawaida kanisa litafanya jambo lile lile. Hivyo, kama nilikuwa nachagua kanisa, ningechagua kanisa halisi, la kimsingi, linaloamini Injili Yote, kanisa la Biblia, kama ningelikuwa nachagua moja la kuingiza familia yangu. Chagua. Niliwaangalia …

25 Wale wavulana, hivi majuzi, mwana wa Ndugu Shakarian na mkwewe, walinipeleka hapa kumwombea jamaa mdogo, mwimbaji, mvulana mzuri. Alikuwa tu amerudi… Fred Barker, hilo ndilo jina lake, alikuwa amerudi tu kutoka safarini. Nao wakanipigia simu, kwamba, "Fred alikuwa anakufa." Ndipo, kabla sijaifikia ile nyumba, ujumbe mwingine ukaja, "Huenda akawa amekufa sasa hivi." Naye akasema alikuwa na ku—kutokwa na damu kwenye ubongo, naye alikuwa amepooza, na—naye alikuwa anakufa, na mke wake alinitaka nimwombee.

Na nikawaza, "Loo, kama nikijaribu kuruka kwa ndege, yeye atakuwa amekufa kabla sijafika kule, na huenda amekufa sasa." Kwa hiyo, nikapiga simu haraka na kumpata maskini mama huyo kwenye simu. Na—na tukaiweka ile simu, kwenye sikio la Fred. Asingeweza kumeza. Walimfanyia ameze kwa kutumia mpira. Na wakati tulipomwombea, akasema, akaashiria, ukatolewa kooni mwake. Angeweza kumeza. Madaktari hawakuamini hilo. Wakautoa, naye angeweza kumeza. Alikuwa ameketi, hivi majuzi.

Kanisa; kuchagua kanisa.

26 Simu iliingia tu, muda mfupi uliopita. Asubuhi hii, mshirika wa kanisa langu, ambaye ni mwanamke Mbatisti hasa kutoka Louisville, alikufa mapema asubuhi ya leo. Na kanisa langu nyumbani, kundi halisi la watu waliowekwa wakfu, walikusanyika pamoja na kushuka kwenda huko, kabla ya mwenye kutayarisha mazishi hajamtia dawa asioze, wakasimama mbele zake, wakaomba hata uhai ukamrudia. Naye yu hai, usiku huu. Wazee wa kanisa langu, mbona, wamefundishwa kuamini ya kwamba mambo yote yanawezekana, wanamjia Mungu kwa uaminifu.

Kwa hiyo, ni lazima ufanye chaguo sahihi.

27 Tena, aina ya mwanamke ambaye mwanamume angemchagua, itaonyesha matamanio yake na tabia yake. Kama mwanamume akimchagua mwanamke asiyefaa, inaonyesha tabia yake. Na kile anachojifunganisha nacho, kinaonyesha kilicho ndani yake kweli. Mwanamke huonyesha kile kilicho ndani ya mwanamume anapomchagua kuwa mke wake. Inaonyesha kile kilicho ndani yake. Haijalishi analosema huko nje, tazama alichooa.

Naenda kwenye ofisi ya mtu fulani, naye anasema yeye ni Mkristo; picha zimebandikwa kote ukutani, ule muziki wa rumba ukiendelea. Sijali yeye anasema nini. Siamini ushuhuda wake, kwa sababu roho yake inakula vitu hivyo vya ulimwengu. Vipi, tuseme, kama angeoa msichana mwimbaji wa bendi, ama vipi kama angeoa kipusa wa watu, ama mrembo tu, mhuni mamboleo? Inaonyesha. Inaonyesha kile alicho nacho katika nia yake, jinsi nyumba yake ya baadaye itakavyokuwa, kwa sababu amemchukua kusudi akawalee watoto wake kwake. Na chochote alicho mwanamke huyo, hivyo ndivyo atakavyowalea hao watoto. Kwa hiyo, inaonyesha kile kilicho ndani ya mwanamume huyo. Mwanamume anayemchukua mwanamke kama huyo, anaonyesha tu kile anachowazia juu ya siku za usoni.

Ungeweza kuwazia Mkristo akifanya jambo kama hilo? La, bwana. Nisingewaza. Mkristo wa kweli hatawatafuta vipusa kama hao, na wasichana waimbaji wa bendi, na vidosho wa watu. Yeye atatafuta tabia ya Kikristo.

28 Sasa, huwezi kuwa na vitu vyote. Huenda kukawa na msichana mmoja ambaye ni mrembo sana. Na yule msichana mwingine, labda yeye ana … kimo chake kinaonekana bora zaidi kuliko huyu. Na huenda ikakulazimu kujinyima mmoja kwa ajili ya huyo mwingine, lakini, kama yeye hana tabia ya mama, ya mwanamke. Na, yeye … Sijali kama yeye ni mrembo au la. Afadhali uangalie tabia yake, awe ni mrembo ama si mrembo.

Sasa, kwa kuwa, inafaa, kama Mkristo angechagua mke, anapaswa kuchagua mwanamke halisi, aliyezaliwa mara ya pili, haidhuru anaonekanaje. Ni kile alicho, ndicho kinachomfanya. Na kisha, tena, hilo linaonyesha tabia yake mwenyewe ya kiungu, na huonyesha kile kilicho katika nia yake na kile kitakachokuwa katika siku za usoni, kwa kuwa familia yake italelewa na mwanamke kama huyo, kwa ajili ya mipango ya siku za usoni ya nyumba yake.

Kama akioa mmoja wa hawa vipusa wahuni mamboleo, vidosho wa watu, angeweza kutarajia nini? Mtu angeweza kutarajia kuwa na nyumba ya namna gani? Kama akimuoa msichana ambaye hana uadilifu wa kutosha kukaa nyumbani na kutunza nyumba, na anataka kufanya kazi katika afisi ya mtu fulani, atakuwa mtunza nyumba wa aina gani? Utakuwa na mayaya na kila kitu kingine. Ni kweli.

29 Sasa, mimi sipendi sana hii tabia ya kisasa, ya wanawake kufanya kazi. Nilipowaona wanawake hawa wakiwa wamevalia hizi sare, wakiendesha katika mji huu, juu ya pikipiki, kama polisi, ni aibu kwa mji wowote ambao utamwacha mwanamke afanye hivyo. Unaona? Unaona? Huku wanaume wengi wakiwa hawana kazi, inaonyesha mawazo ya kisasa ya mji wetu. Inaonyesha kushuka kwa uadilifu. Haitupasi kuwa na hao wanawake huko nje namna hiyo. Hawana shughuli zozote huko nje namna hiyo.

Wakati Mungu alipompa mwanamume mke, Yeye alimpa kitu kilicho bora zaidi angeliweza kumpa, nje ya wokovu. Lakini wakati mmoja anapojaribu kuchukua mahali pa mwanamume, basi yeye ni karibu kitu kibaya kuliko vyote ambavyo angeweza kupata. Sasa, hiyo ni kweli. Unaona?

Sasa tunaweza kuona matumizi ya kiroho.

Na—najua hiyo ni mbaya, unafikiri ni mbaya, bali ni Kweli. Hatujali ni mbaya jinsi gani, hatuna budi kukabiliana na jambo lilivyo. Hivyo ndivyo Biblia inavyofundisha. Unaona?

30 Sasa, sisi hapa tunaona dhahiri mpango wa kiroho, wa mpango wa Mungu kwa ajili ya Makao Yake ya usoni pamoja na Bibi-arusi Wake wa baadaye, ukionekana sasa.

Kama mwanamume akioa kidosho wa watu, unaona kile anachotazamia siku za usoni. Kama mwanamume akioa mwanamke ambaye hatakaa nyumbani, unaona kile anachotazamia katika siku za usoni. Na mimi wakati mmoja …

Hili linasikika kuwa baya sana. Najisikia tu kusema jambo hilo. Nami—nami, kwa kawaida, kama ninajisikia kusema jambo hilo, inanipasa kulisema. Na kwa kawaida huwa ni njia ya Mungu.

Ni—nilizoea kwenda kwa mfugaji niliyefanya naye kazi, kununua ng'ombe. Nami nikamwona yule jamaa mzee kila mara akiangalia moja kwa moja katika usoni mwa mtamba wa ng'ombe kabla hajaenda kumnadia. Kisha akakigeuza kichwa chake, na kumwangalia huku na huko. Nilimfuata, nikamwangalia. Naye akamwangalia juu chini, kama alionekana sawa, kwa umbo. Ndipo akageuka akamwangalia usoni, na wakati mwingine angetikisa kichwa chake na kuondoka.

Nikasema, "Jeff, nataka kukuuliza jambo fulani."

Akasema, "Sema, Bill."

Nami nikasema, "Kwa nini kila mara unamtazama ng'ombe huyo usoni?" Nikasema, "Anaonekana sawa, ng'ombe mzuri—mzito."

Kasema, "Nataka kukwambia, ewe mvulana, una mengi ya kujifunza." Nami ni—nilitambua jambo hilo baada ya yeye kuniambia. Kasema, "Sijali alivyoumbika. Huenda akawa amejaa nyama sana, mpaka kwenye kwato. Lakini kama yeye ana hayo macho jeuri usoni mwake, usimnunue kamwe."

Nikasema, "Mbona hivyo, Jeff?"

"Vema," kasema, "jambo la kwanza ni kwamba," kasema, "yeye hatatulia kamwe." Naye akasema, "Jambo la pili ni kwamba, hatakuwa mama kamwe kwa ndama wake." Kisha akasema, "Wanamweka zizini sasa, ndiyo sababu yeye ni mnono. Hebu mfungulie, akiwa na hayo macho jeuri, angetimua mbio hadi afe."

Nikasema, "Unajua, kwa namna fulani nimejifunza jambo fulani. Naamini hilo linawahusu wanawake, pia." Sawa. Sawa.

Hayo macho jeuri, yanayong'ara, ya kihuni, afadhali usimkaribie, ewe mvulana, vitu hivyo vyote vyenye rangi ya bluu juu ya macho yake. Nami sikuninii … Nisingevitaka hivyo. Sidhani hivyo vinafaa kwa Mkristo. Sijali ni kiasi gani televisheni na magazeti yanavyosema ni virembo. Ndicho kitu cha kuchukiza kuliko vyote, cha kutisha mno nilichowahi kuona maishani mwangu.

31 Nilipoviona hivyo kwa mara ya kwanza, hapa kwenye Hoteli ya Clifton, asubuhi moja, kwenye kiamshakinywa. Niliwaona baadhi ya hao wasichana wakija. Ndugu Arganbright alikuwa ndiyo kwanza aingie, na mimi. Naye alikuwa ameshuka kwenda orofa ya chini. Nami nikaangalia, na huyo msichana

akaingia. Nikawaza, "Vema, si—si—si—sijui." Sijapata kuiona hapo kabla. Ilikuwa ni ya aina fulani. Loo, ilionekana kana kwamba alikuwa ameoza, mnajua, kwa namna fulani alionekana wa kuchekesha. Sisemi jambo hilo ili kuchekesha. Na—ninasema jambo hilo. Mnajua, nimeona ukoma. Mimi ni mmishenari. Niliona kila namna ya vituko, mnajua, jinsi magonjwa yalivyo. Nami nilikuwa niende kwa msichana huyo na kumwambia, "Mi—mi—mimi ni mhudumu. Ni—nawaombea wagonjwa. Ungetaka—ungetaka nikuombee?" Nami sikuwa nimewahi kuona kitu kama hicho. Na halafu, hawa hapa wakau ja wawili awatatu zaidi, wakaingia. Kwa namna fulani nilirudi nyuma wakati huo nikangojea.

Na Ndugu Arganbright akaja pale, kwa hiyo nikasema, "Ndugu Arganbright?" Huenda akawa hapa. Nikasema, "Yule mwanamke ana shida gani?" Unaona?

Naye akasema, "Hiyo, hiyo ni rangi."

Nikasema, "Vema, jamani, jamani!" Unaona? Nilifikiri wangepaswa kumweka katika hospitali ya maradhi mabaya mahali fulani, mnajua, asije akawaambukiza wanawake wengine wote.

32 Lakini, unajua, inakupasa kupanga, kuangalia, kuomba, wakati unachagua. Kwa kuwa, tunaona, kwa hili, Neno la ahadi. Yeye, bibi-arusi ambaye mwanamume angemchagua, ataonyesha tabia yake. Inaonyesha yaliyo ndani yake.

Sasa, ungeweza kuwazia mwanamume, aliyejazwa na Roho Mtakatifu, akichukua kitu kama hicho kuwa mke? [Kusanyiko linasema, "La." — Mh.] Mimi—mimi—mimi sioni jambo hilo, ndugu. Sasa, labda mimi ni mzee tu. Lakini, unajua, si—siwezi kufelewa jambo hilo, unaona, angalia, kwa kuwa litaonyesha kile kilicho ndani yake. Huyo atamsaidia kutengeneza makao yake ya siku za usoni.

Sasa, basi, tunapogeukia sasa kwa muda mfupi, kwenye upande wa kiroho. Na wakati unapoona kanisa ambalo liko ulimwenguni, likitenda kama ulimwengu, likitazamia ulimwenguni, likishiriki ya ulimwengu, likizihesabia Amri za Mungu kana kwamba kamwe Yeye hakuziandika, ndipo u—unaweza tu kuwazia kwamba Kristo hataenda kumchukue Bibi-arusi kama huyo. Je, ungeweza kuwazia kuchukuliwa kwa hili kanisa la kisasa leo hii kama Bibi-arusi? Si Bwana wangu. Mimi si … Ni vigumu kwangu kuona hilo. Hapana. Kumbuka, sasa, mwanamume na mkewe ni mmoja. Je! Ungelijiungamanisha mwenyewe na mtu kama huyo? Kama ungelifanya hivyo, bila shaka kwa namna fulani lingelivunja imani yangu kwako.

33 Na, basi, vipi kuhusu Mungu kujiunganisha na kitu kama hicho, kahaba wa kawaida wa kidhehebu? Mnafikiri angefanya hivyo, "Wenye mfano wa utauwa lakini wakikana nguvu zake"? Yeye hangefanya hivyo kamwe. Hana budi kuwa na tabia Yake ndani yake. Kanisa halisi, la kweli lililozaliwa mara ya pili halina budi kuwa na ile—ile tabia iliyokuwa ndani ya Kristo, kwa sababu mume na mke ni mmoja. Na kama Yesu alifanya tu yale yaliyompendeza Mungu, akalitimiza Neno Lake na kulidhihirisha Neno Lake, itampasa Bibi-arusi Wake kuwa wa tabia ya aina ile ile. Bibi-arusi asingeweza, kwa vyo vyote vile, kuwa dhehebu. Kwa sababu, basi, haidhuru ni kiasi gani unataka kusema, "hapana," hilo linaongozwa na halmashauri mahali fulani, ambayo huliambia litende nini na lisitende nini, na, mara nyingi, huwa umbali wa maili milioni moja kutoka kwenye Neno la kweli.

34 Ni vibaya sana kwamba tuliondoka kwa yule Kiongozi halisi ambaye Mungu alituachia kuliongoza Kanisa. Yeye kamwe hakuwatuma wazee wa jimbo. Yeye kamwe hakutuma maaskofu, makadinali, makasisi, mapapa. Yeye alimtuma Roho Mtakatifu kwa ajili ya Kanisa, kuliongoza Kanisa. "Wakati Yeye Roho Mtakatifu atakapokuja, atawaongoza katika Kweli yote, awafunulie mambo haya, ambayo nimewaambia, atawakumbusha, na kuwaonyesha mambo yajayo." Roho Mtakatifu alikuwa afanye hivyo. Sasa, kanisa la kisasa linamchukia Huyo. Hawamtaki Huyo, kwa hivyo lingewezaje kuwa Bibi-arusi wa Kristo? Watu wa siku hizi wanachagua dhehebu la kisasa. Linachofanya, linaonyesha tu ufahamu wao duni wa Neno.

Sikusudii kuudhi, bali namaanisha iingie ndani vya kutosha hata uichunguze.

35 Nimewaoza wanandoa wengi, lakini daima hunikumbusha juu ya Kristo na Bibi-arusi Wake. Moja ya arusi ambazo nilifanya hapa, wakati fulani uliopita, ilikuwa—ilikuwa ni jambo kuu sana maishani mwangu. Imekuwa miaka kadha iliyopita, nilipokuwa tu mhudumu kijana.

Ndugu yangu alikuwa akifanya kazi kwenye—kwenye P.W.A. Sijui kama mtu ye yote anakumbuka jambo huo, bado, ama la, mtu ye yote aliye mzee kama mimi. Na huo ulikuwa m—mradi ambao serikali ilikuwa nao. Na ndugu yangu alifanya kazi kule, yapata maili thelathini hivi. Walikuwa wakichimba maziwa fulani, mradi wa uhifadhi.

Na kulikuwa na mvulana mmoja aliyefanya kazi huko, pamoja naye, kutokea Indianapolis, yapata, loo, yapata maili mia moja juu ya Jeffersonville ambako ni—ninaishi, ama nilikoishi. Na kulikuwako na … Yeye alimwambia ndugu yangu, siku moja, akasema, "Doc," akasema, "Na—nataka … Nitaoa, kama tu ningelikuwa na fedha za kutosha kumlipa mhubiri." Akasema, "Nina—nina fedha za kutosha kugharimia hati yangu, lakini," kasema, "Sina fedha za kutosha kumlipa mhubiri."

Doc akasema, "Vema, ndugu yangu ni mhubiri, na—na a—anaweza kukuoza." Yeye akasema, "Yeye kamwe hawalipishi watu kwa ajili ya mambo kama hayo."

Akasema, "Je! Utamwuliza kama ataniozesha?"

36 Vema, usiku huo ndugu yangu akaniuliza. Nikasema, "Kama hajawahi kuoa huko nyuma, mmoja wao hao wawili, nao ni … kila kitu kiko sawa." Akasema, "Vema, naam, nitamwuliza." Nami nikasema, "Kama ndivyo ilivyo, mwambie, aje huku."

Kwa hiyo, Jumamosi ilipofika ndipo mvulana huyo akaja. Limekuwa ni jambo kuu kwangu, kukumbuka jambo hili daima. Ninge … Alasiri yenye mvua, na gari la zamani la Chevrolet, likiwa na mataa yake yaliyoshikiliwa kwa waya, ikaja moja kwa moja, hapo mbele. Muda mfupi tu baada ya kumpoteza mke wangu, nami nilikuwa nikiishi kama kapera, vyumba viwili vidogo. Na—na Doc alikuwa huko pamoja nami, tukiwangojea.

Na—na mvulana mmoja akatoka kwenye gari lile, naye hakika hakuonekana kama bwana-arusi, kwangu mimi, ama kwa yeyote yule, nadhani. Naam. Ningeweza ku … kununua jozi nzuri ya viatu, kwa dola moja na nusu. Naye alikuwa amevalia jozi, iliyochakaa kabisa. Na suruali yake ilikuwa yenye kupwaya mno. Naye alikuwa amevaa moja ya haya makoti ya kale ya ngozi za fuko. Sidhani baadhi yenu ninyi wazee mngeweza kukumbuka. Lilionekana kana kwamba lilikuwa limepitishwa kwenye mtambo wa kufulia nguo bila kukamuliwa, nalo lilikuwa na milia, limefungwa namna *hii*, pembeni juu.

37 Ndipo bibiye mdogo fulani akatokea upande mwingine, akiwa amevalia ninii ndogo, loo, baadhi ya mavazi hayo madogo yenye miraba.

Sijui. Nilikosea kuita aina hiyo ya kitambaa, wakati mmoja. Gingham, naamini ndivyo kinavyoitwa. Na kwa hivyo ilikuwa … [Kusanyiko linacheka — Mh.] Nilikisema vibaya tena. Mimi—mimi daima hufanya hivyo. Nami nikasema …

Akatoka kwenye gari ile, nao wakapanda kwenye vipandio. Na—na wakati walipoingia ndani, maskini msichana yule, yeye … Nadhani, yeye, karibu yote aliyokuwa nayo tu ni sketi. Naye hakuwa na viatu, hata miguuni. Alikuwa amesafiri kwa miguu kutokea Indianapolis huku akiomba lifti, akija. Alikuwa na nywele ndogo zilizoning'inia chini, mgongoni, katika misuko mirefu, iliyoning'inia mgongoni mwake. Alionekana mchanga sana.

Nami nikamwambia, "Je! Wewe umetosha umri wa kuolewa?"

Akasema, "Naam, bwana." Naye akasema, "Nina ruhusa yangu iliyoandikwa kutoka kwa baba na mama yangu." Akasema, "Ilinibidi kuionyesha kwa—mahakamani hapa, ili nipate hati yangu."

Nikasema, "Vema." Nikasema, "Ningetaka kuzungumza nanyi kidogo kabla ya kufanya hii harusi." Wakaketi. Mvulana huyo aliendelea kuangalia huku na huko chumbani; alihitaji kukata nywele vibaya sana. Naye akaendelea kutazama huku na huko chumbani. Hakuwa akinisikiliza. Nikasema, "Mwanangu, nataka usikilize yale ninayosema."

Kasema, "Naam, bwana."

Nami nikasema, "Je, unampenda msichana huyu?"

Akasema, "Naam, bwana. Nampenda."

Nikasema, "Nawe unampenda?"

"Naam, bwana. Nampenda."

Nikasema, "Sasa, una mahali pa kumpeleka baada ya kumuoa?"

Kasema, "Naam, bwana."

Nikasema, "Vema. Sasa," nikasema,"nataka kuwaulizeni jambo fulani. Nasikia, unafanya kazi juu hapa kwenye hii P.W.A."

Naye akasema, "Naam, bwana." Hiyo ni kama dola kumi na mbili kwa wiki.

Nikasema, "Unafikiri unaweza kumpatia riziki?"

Akasema, "Nitafanya yote niwezayo kufanya."

Nami nikasema, "Vema, hiyo ni sawa." Nami nikasema, "Sasa, vipi kama akiondoka kwenye … Vipi kama akipoteza kazi hii, dada? Utafanya nini, utakimbia kurudi nyumbani, kwa mama, baba?"

Yeye akasema, "La, bwana. Nitadumu pamoja naye."

Nami nikasema, "Vipi, bwana, kama unao watoto watatu ama wanne, huna kitu cha kuwalisha, na huna kazi yo yote. Utafanya nini, utamfukuza?"

Kasema, "La, bwana. Nitakazana zaidi. Tutafaulu, kwa vyovyote vile."

Nilijisikia mdogo. Nami nikaona ya kwamba kweli alimpenda huyo msichana, nao walipendana. Nikawaoza.

38 Ndipo nikashangaa mahali alikompeleka. Siku chache, nilimwuliza ndugu yangu, Doc, kuwa ni wapi. Akasema, "Nenda kule New Albany," mji mdogo chini yetu.

Na huko chini mtoni, ambako nilikuwa nimeweka mabati, nilikoenda kila siku wakati ni—nilipokuwa mchunguzi wa nyaya za nguvu za umeme. Kwa hiyo wakati hao watu wengine, hao wote wanapoketi chini, wakisema mizaha na kadhalika, ningeingia ndani ya gari na kukimbia mtoni na kuomba wakati huo …? Nami ninasoma Biblia yangu, chini ya kipande kikubwa cha bati ambapo kiwanda cha chuma kilikuwa. Kuna mabehewa makuu-kuu kule.

Na jamaa huyu alikuwa amekwenda kule na kujitwalia moja ya haya mabehewa na kujitengenezea mlango ndani yake. Na alikuwa amechukua gazeti na misumari yenye kofia.

Ni wangapi wanaojua msumari wenye kofia? Hakuna Wakentucky hapa, basi. Ni, chukua kipande cha kadibodi, kitie kijikofia, msumari bapa. Na halafu ukipigilie ndani ya … Huo ndio msumari wenye kofia.

39 Hivyo, walikuwa wameiweka kote. Naye alikuwa amepanda kwenda kule kwenye kiwanda cha chuma na kujiokotea vikorokoro, na kujitengenezea kipandio, cha kupandia. Na akaokota masanduku yaliyochakaa, na kujitengenezea meza. Nami nikawaza, siku moja, "Nitashuka niende nikaone jinsi wanavyoendelea."

Yapata miezi sita kabla ya hapo, nilimwoza binti wa E. V. Knight na mwanawe E. T. Slider. E. V. Knight, mmoja wa watu walio matajiri sana walioko kwenye Mto Ohio, na, loo, husimamia viwanda vikubwa huko, vya kutengenezea nyumba hizi za kuunganishwa, na kadhalika. Na—na Slider, E. T. Slider, ana kampuni ya mchanga na changarawe, watoto wa mamilionea. Nami nilikuwa nimewaoza.

Nami nikarudi mahali fulani, nikajizoeza hayo kwa yapata muda wa wiki mbili, na kurudi kwenye kibanda na kupiga magoti kwenye mto. Na sherehe zote na kila kitu nilichowahi kupitia, karibu, yalinipasa kupitia, kusudi nikawaoze hao wawili! Na wakati walipojitokeza, mbona, walikuwa … Hawa wanandoa wengine wadogo walisimama tu pale katika chumba kidogo kikuu-kuu ambapo tulikuwa na kitanda kidogo cha kupumzikia na kitanda kilichokunjwa, lakini wote walikuwa wameozwa kwa sherehe ile ile.

40 Ndipo basi, siku moja, nilifikiri ningeenda huko chini na kuwatembelea hawa mume na mke matajiri. Haikuwalazimu kufanya kazi, baba zao walikuwa ni mamilionea, walikuwa wamewajengea nyumba nzuri. Kwa kweli, huyu E. V. Knight, juu, hapa kilimani, vinundu vya milango yake vina kipimo cha kumi na nne cha dhahabu kwenye jumba lake kubwa, kwa hiyo unaweza kuwazia wanaishi katika nyumba ya namna gani. Haikuwalazimu kufanya kazi. Walikuwa wamepewa Cadillac nzuri kila mwaka. Na ni, watoto tu, nao walikuwa na kila kitu walichotaka. Wakati nilipotembea huko siku moja …

Sasa, jinsi nilivyowafahamu, mmoja wa marafiki zao alikuwa rafiki yangu mzuri. Ni kama sisi sote tuliunganika pamoja. Na hivyo ndivyo nilivyofahamiana nao, wakati walipotaka niwaoze.

41 Kwa hiyo nikaenda kuwatembelea. Nilitoka nje ya Ford yangu ya kale, nje, nikapanda vipandio. Na—na nikafika, karibu sana, nami nikawasikia. Nao walikuwa wakizozana vikali. Walionena wivu. Walikuwa wamehudhuria kwenye dansi. Yeye alikuwa msichana mrembo sana. Naye kwa namna fulani alikuwa mmoja wa hawa malkia wa urembo. Alishinda tuzo nyingi sana kule, na kujishindia magari na kadhalika, kwa kule kuwa malkia wa urembo. Nami nikawaangalia, na mmoja alikuwa ameketi kwenye kona moja na mwingine kona nyingine, wakizozania mvulana fulani aliyekuwa amecheza dansi naye, ama msichana fulani, kitu fulani.

Nilipokuja, waliruka upesi sana na kushikana sakafuni, na mikono yao—yao, sakafuni, wakaja wakielekea mlangoni. Kasema, "Naam, u hali gani, Ndugu Branham! Unaendeleaje?"

Nikasema, "Vema. Mnaendeleaje nyote?"

Na, "Loo," mume akasema, "Mimi—mimi … Tuna furaha sana. Sivyo, mpenzi?"

Naye mke akasema, "Naam, mpenzi." Unaona?

42 Sasa, unaona, unajivika kitu ambacho si halisi. Sasa, huwezi kupata joto kwa moto uliochorwa, kama baadhi ya makanisa haya yanayojaribu kuchora pentekoste, ya kitu kilichotukia miaka elfu moja iliyopita ama miaka elfu mbili iliyopita. Huwezi kupata joto kwa moto uliochorwa. Pentekoste ni halisi tu leo kama ilivyokuwa wakati ule. Unaona? Naam. Ule Moto ungali unashuka. Si moto wa kuchorwa. Ni Moto halisi.

Hivyo, wao, hao tu hapo. Unaona? Ni—nisingetaka kuishi namna hiyo.

43 "Loo," nikawazia, "unajua, huko chini tu kwenye lile genge kule kule mtoni, hapo ndipo hawa wengine wawili walikokwenda." Nikawaza, "Jumamosi moja alasiri ningejipenyeza kule na kuona jinsi walivyokuwa wanaendelea."

Kwa hiyo mimi, nikiwa mchafu usoni, na nimevaa ovaroli chafu, nimebeba zana zangu. Nikawaza, "Nitawatembelea kisiri." Nilijipenyeza kwa siri kana kwamba nilikuwa nikichunguza mipira ya kufunika nyaya za nguvu za umeme zilizokatwa na radi ama kitu fulani, na huku nikitembea kando ya waya wa simu, nyaya za umeme kando ya mto. Na ile pale Chevrolet iliyochakaa, ilikuwa mbele ya nyumba. Yapata mwaka mmoja baadaye, baada ya kuwaoza. Na kulikuwako na—na … Mlango ulikuwa wazi, nami niliweza kuwasikia wakizungumza. Kwa hiyo hili linasikika kama mnafiki, bali nilisogea karibu vya kutosha hata ningeweza kusikiliza, kuona yale waliyokuwa wakisema. Nilisimama pale. Nami ninataka tu kujua, mimi mwenyewe.

Napenda kuchunguza na kuwa na hakika ninajua yale ninayozungumzia. Hivyo ndivyo ninavyofanya kuhusu Neno la Mungu. Je! Hilon ni Kweli, ama si Kweli? Je! Yeye atatimiza Neno Lake, ama Yeye halitimizi Neno Lake? Kama Yeye hatimizi Neno Lake, basi Yeye si Mungu. Unaona? Yeye hutimiza Neno Lake, Yeye ni Mungu. Unaona?

44 Na kwa hiyo nataka kuona jinsi walivyokuwa wakiendelea. Nami nikanyemelea kandokando, polepole sana. Nilimsikia mume akisema, "Loo, mpenzi, nilitaka kukununulia hiyo, sana."

Mke akasema, "Sasa, angalia, mpenzi." Akasema, "Nguo hii inatosha." Akasema, "Mbona, hii ni nzuri tu." Kasema, "Nashukuru kwa hilo. Lakini unaona …"

Nilijipenyeza pale, ili niweze kuangalia ndani kupitia kwenye mwanya, ambapo mlango ulikuwa umefunguliwa kule kwenye lile behewa. Naye huyo hapo, akiwa ameketi mle ndani, na mkewe pajani mwake; na amemkumbatia, naye mkewe amemkumbatia. Naye alikuwa na moja ya hizi kofia za kale kama karai, na alikuwa ametoboa kishimo kidogo, akaibonyeza ndani, sehemu ya juu, naye akatoa mshahara wake ndani humo. Yeye—yeye alikuwa ameziweka mezani. Kasema, "*Hizi* ni za vyakula. *Hizi* ni za bima. Na *hizi* ni za gari." Wala hawangeweza kukidhi mahitaji yao. Nikaja kujua, alikuwa ameona gauni dogo huko dukani, amekuwa amelitazama-tazama kwa wiki kadha, ambalo liligharimu dola moja na kitu. Alitaka kulinunua. Kasema, "Vema, mpenzi, ungeonekana mrembo sana ndani yake." Naye akasema …

Naye akasema, "Lakini, mpenzi, ni—ninalo gauni. Mimi—mimi kwa kweli silihitaji." Unaona? Na maskini malkia huyo mdogo …

45 Nikarudi nyuma, na kutazama juu. Ningeweza kuona ninii—mnara juu ya ile nyumba nyingine. Nilisimama pale na kuangalia, dakika chache. Nikawaza, "Ni nani huyo tajiri?" Nikawazia, "Kama, Bill Branham, kama unataka kuchukua mahali, ungeenda wapi?" Kwangu mimi, nisingechukua kile kitu cha kupendeza kule juu ya kilima. Ningemchukua mtu huyu hapa chini, kama mjenzi halisi wa nyumba, mtu fulani aliyenipenda na kukaa pamoja nami, mtu fulani alijyearibu kujenga nyumba; na si kukukamua kwa kila kitu, kwa ajili ya umaridadi; na mtu aliyekuwa pamoja nawe, aliye sehemu yako.

46 Hiyo daima imedumu nami, ya jinsi hayo yalivyokuwa. Mmoja alimchagua msichana mrembo, huyo mwingine alichagua tabia. Sasa, hiyo tu ndiyo unavyoweza kuchagua. Kwanza, tafuta tabia na, kisha, kama unampenda. Vema.

Angalia, Adamu wa kwanza wa Mungu hakuwa na chaguo lo lote, kwa ajili ya mkewe. Hakupata chaguo. Mungu alimfanya tu mmoja, naye hakupata kumchagua. Kwa hiyo tunaona ya kwamba alimwongoza vibaya mbali na Neno la Mungu. Yeye hakupata kuombea jambo hilo. Yeye—yeye—yeye si kama wewe na mimi. Hakupata chaguo. Na tena, kwa kufanya hivyo, yeye alimwondoa mbali na mahali pake panapofaa kama mwana wa Mungu. Naye alifanya hivyo kwa kumwonyesha njia ya kisasa zaidi ya maisha, jambo ambalo kwa kweli hawakupaswa kufanya. Lakini tabia yake ilionyesha ya kwamba mke alikuwa amekosea. Malengo yake na makusudi yake yalikuwa mabaya tu. Na akamshawishi, kwa hoja yake, ya kwamba ile nuru mpya ya kisasa aliyokuwa amepata, ambayo ilikuwa ni kinyume cha Neno la Mungu, ilikuwa njia bora zaidi ya kuishi.

47 Na ni wanawake wangapi leo, na vinginevyo, wanaume, ambao wangeweza kumwondosha mwanamke mzuri kwa Mungu, ama kumwondosha mwanamume mzuri kwa Mungu, kwa kujaribu kumwambia, "Dini hii, enyi wavulana wa Kipentekoste! Dini hiyo," wao husema,"loo, Hiyo ni ya mtindo wa kale. Ni ukungu wa kale. Usiiamini Hiyo." Ni bora uombe kwa bidii kabla hujamwoa msichana huyo. Sijali yeye ni mrembo jinsi gani. Vivyo hivyo kwa mwanamume.

Yeye alimshawishi atoke kwenye mapenzi ya Mungu na kumfanya atende jambo ambalo hakupaswa kutenda, na, kwa hilo, likasababisha mauti kwa jamii yote ya binadamu. Hiyo ndiyo sababu Biblia inamkataza kufundisha, ama kuhubiri, ama kulishughulikia Neno la Mungu, kwa njia yo yote.

Ninajua, dada, wengi wenu husema, "Bwana aliniita kuhubiri."

Sitabishana na wewe. Lakini nitawaambia, Neno linasema haikupasi kufanya hivyo. "Hatafundisha, wala kuntwaa mamlaka yo yote, bali awe katika ukimya."

"Vema," unasema, "Bwana aliniambia nifanye hivyo."

Sitilii shaka hilo hata kidogo. Je, mlisikia Ujumbe wangu hivi majuzi usiku kuhusu Balaamu? Balaamu alipata uamuzi wa kwanza, waziwazi wa Mungu, "Usifanye hilo." Lakini aliendelea kujipumbaza hata mwishowe Mungu akamwambia aende akatende jambo hilo.

Huenda Mungu akakuruhusu kuhubiri. Sisemi Yeye hakufanya hivyo. Lakini si kulingana na Neno Lake la asili na mpango Wake. "Kwa maana anapaswa kutii, kama isemavyo torati." Ni kweli. Kwa hiyo, yeye hapaswi kufanya hivyo.

48 Sasa, angalia tena jinsi bibi-arusi wa kawaida alivyo mfano wa kiroho. Neno linasema, ya kwamba, "Mwanamke aliumbwa kwa ajili ya mwanamume, wala si mwanamume aliyeumbwa kwa ajili ya mwanamke."

Sasa nitazungumza, na kwa nini, katika dakika chache, juu ya Bibi-arusi wa Kristo, lakini ninajaribu kuwaonyesha msingi wake.

"Mwanamke aliumbwa kwa ajili ya mwanamume, na si mwanamume kwa ajili ya mwanamke." Hiyo ndiyo sababu, chini yatorati ya kale, ambapo kuoa wanawake wengi kulikuwa halali. Mwangalie Daudi akiwa ameketi kule chini akiwa na wake mia tano, na Biblia ilisema, "Yeye alikuwa mtu aliyeupendeza moyo wa Mungu." Akiwa na wake mia tano, na Solomoni akiwa na elfu moja, lakini hakuna hata mmoja wa hao wanawake angeliweza kuwa na mume mwingine.

49 Chukueni kanda yangu ya *Ndoa Na Talaka*. Ambapo, juu ya mlima kule Tucson, hapa si muda mrefu uliopita, nilikuwa huko juu nikiomba juu ya jambo hilo. Wao waliwaruhusu wanafunzi waondoke shuleni, ili waangalie ile Nguzo ya Moto ikiuzunguka ule mlima na kufanya umbo la faneli, mbele na nyuma, juu na chini. Watu wa karibu hapa wanajua jambo hilo, hapo, na wakaiona; Nayo ilininii … wakati aliponiambia Ukweli wa maswali haya ya ndoa na talaka. Kama kuna upande mmoja unaokwenda upande *huu*, na mmoja ukienda upande *ule*, hapana budi kuwe na Kweli mahali fulani. Baada ya ile Mihuri Saba, Yeye alionyesha Ukweli wake ulivyo.

50 Angalia, sasa, mwanamke asingeweza kuwa na zaidi ya mume mmoja, kwa sababu, "Mwanamke alifanyika kwa ajili ya mwanamume, na si mwanamume kwa ajili ya mwanamke." Hao wanawake wote mia tano walikuwa tu ni mke wa Daudi, na hilo lilikuwa ni mfano. Wakati Kristo atakapoketi kwenye Kiti cha Enzi katika ule Utawala wa Miaka Elfu, Bibi-arusi Wake hatakuwa mtu mmoja, bali itakuwa ni makumi ya maelfu, Bibi-arusi, wote katika Mmoja. Naye Daudi alikuwa na wake wengi, kama watu binafsi, lakini wote tu pamoja walikuwa mke wake. Kama vile Mwili wote wa waamini ulivyo Bibi-arusi wa Kristo, maana ni Yeye, mwanamke. Yeye alikuwa Mwanamume. Sasa, sisi tulifanywa kwa ajili ya Kristo. Kristo hakufanyika kwa ajili yetu.

Hilo ndilo tunalojaribu kufanya leo katika vitabu vyetu vya kiada, ni kujaribu kulifanya Neno (ambalo ni Kristo) litufae sisi, badala ya sisi kujaribu kujifanya wanaofaa kwa Neno. Hiyo ndiyo tofauti.

51 Wakati mwanamume anapomchagua msichana fulani kutoka kwa familia fulani, yeye hapaswi kutegemea urembo, kwa kuwa uzuri hudanganya. Na uzuri, uzuri wa kisasa wa kilimwengu, ni wa ibilisi.

"Loo," namsikia mtu fulani akisema huko nje, "uwe mwangalifu hapa, mhubiri!"

Nasema ya kwamba mambo haya hapa duniani, ambayo yanaitwa marembo, ni ya ibilisi kabisa. Nitawathibitishia jambo hilo. Halafu, kwa minajili ya tamshi hili, hebu tuchunguze Neno takatifu la Mungu, tuone kama hilo ni kweli ama si kweli. Na baadhi yenu ninyi wanawake mnataka kuwa warembo sana! Angalia unakotoka. Hapo mwanzo, tunaona ya kwamba Shetani alikuwa mrembo sana hata akawadanganya Malaika. Naye alikuwa Malaika mwenye sura nzuri sana kuliko wengine wote. Ilionyeshwa, inatokana na Ibilisi. Mithali ilisema, Solomoni alisema, "Uzuri unapita upesi." Hiyo ni kweli. Dhambi ni maridadi. Hakika, ndivyo ilivyo. Inavutia.

52 Nataka kuwaulizeni, na kuwaambia jambo fulani hapa. Nawatakeni mwone, dakika chache. Kati ya spishi zote ulimwenguni, ndege, wanyama, tunaona ya kwamba kwenye maisha ya wanyama, wote isipokuwa mwanadamu, ni wa kiume aliye maridadi, na si wa kike. Mbona hivyo? Mwangalie naninii … Mwangalie yule kulungu, m—dume mkubwa mzuri mwenye pembe zake, na maskini jike lake kaidi. Mwangalie ku—kuku, kuku mdogo, mwenye madoadoa, na jogoo mkubwa mwenye manyoya mazuri. Mwangalie ndege wa kiume na ndege jike. Mwangalie bata mwitu wa kiume na wa kike. Unaona? Na hakuna spishi hata moja ulimwenguni, iliyoumbwa, iwezayo kudanganya na kujidunisha kama mwanamke.

Sasa, dada, usisimame na kutoka nje. Ngojeni tu mpaka tutakaposikia mwisho wa Hili. Unaona?

Unaona?

Hakuna kitu, hakuna jike mbali na mwanamke, linaloweza kuwa zinifu. Mnamwita mbwa "mzembe," mnamwita nguruwe mwitu "ji—jike," lakini, kimaadili, wana uadilifu zaidi ya nusu ya wachezaji mashuhuri wa sinema walioko hapa. Hawawezi kuwa kitu kingine chochote kile ila waadilifu.

53 Na mwanamke alikuwa ndiye aliyebadilishwa, kwa ajili ya upotovu. Hiyo ni kweli. Unaona kule urembo huyo anakompeleka? Sasa, hiyo ndiyo sababu kwamba, leo, tunaona ya kwamba wanawake wanaongezeka uzuri. Mchuke Pearl Bryan, je, mliwahi kuona picha yake? Alidhaniwa kuwa ni mrembo mkuu wa Marekani. Hakuna mtoto yeyote wa shule kutoka shule yo yote ambaye hangelimweka kwenye safu ya nyu-nyuma. Je! Mlijua kwamba inapaswa kuwa hivyo? Je! Mlijua Biblia inasema ya kwamba hivyo ndivyo itakavyokuwa?

Je! Unajua kule kuanguka kulikuja kwa njia ya wanawake hapo mwanzo? Na kuanguka … Mwisho utamalizikia vivyo hivyo, wanawake wakiingia mamlakani na kuwatawala wanaume, na kadhalika. Mnajua Maandiko yanasema hivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Mnajua, siku atakapovaa nguo za mwanamume, na kukata nywele zake, mambo hayo yote ni kinyume na Neno la Mungu. Na je, mnajua yeye anawakilisha kanisa? ["Naam."] Unapoangalia yale wanawake wanayofanya, mtaona yale kanisa linayofanya. Hiyo ni kweli kabisa. Sasa, sasa, hiyo ni kweli tu kama Neno la Mungu lilivyo kweli.

54 Hakuna jike lingine lililofanywa ambalo linaweza kujishusha kama mwanamke awezavyo kujishusha. Na hata hivyo, kupitia hapo, kwa ajili ya kufanywa kutoka …

Yeye hakuwa katika ule uumbaji wa asili. Majike wengine wote walikuwa katika uumbaji wa asili: ndege, wa kiume na wa kike; wanyama, wa kiume na wa kike. Lakini, katika maisha ya mwanadamu, Mungu alimuumba mwanamume pekee, Naye akamtwaa kutoka kwake. Na mwanamke ni kiumbe kilichotoka kwa mwanamume, kwa sababu Mungu hakuanzisha kitu kama hicho. Yachunguzeni Maandiko. Sawa kabisa. Mungu, la, bwana, katika uumbaji Wake wa asili. Alikuwa aliwekwa nje kule.

Lakini kama anaweza kusimama imara, ni thawabu kuu jinsi gani aliyo nayo kuliko mwanamume. Mwanamke amewekwa kwenye uwanja wa majaribio. Kupitia kwake kukaja mauti. Yeye ana hatia ya vifo vyote. Lakini basi Mungu akageuka na kumtumia mmoja kurudisha Uzima tena; alimleta Mwanawe kupitia kwa mwanamke, aliye mtiifu. Lakini alye mbaya ni m—mwovu sana kuliko kilichopo; hakuna kitu kinachoweza kuwa duni hivyo.

55 Kaini, mwana wa Shetani, alidhani ya kwamba Mungu alikubali urembo. Anadhani hivyo leo hii. Kaini alikuwa mwana wa Shetani. "Loo, sasa!" unasema. Hatutafafanua jambo hilo kwa kina, lakini hebu niwafahamishe ninyi. Biblia ilisema ya kwamba yeye "alikuwa wa yule mwovu." Kwa hiyo, hilo latosha. Vema. Sasa, yeye alikuwa mwana wa Shetani. Naye aliwaza kwamba, akileta madhabahu na kuifanya ipendeze sana kwa ajili ya ibada, hilo ndilo Mungu angeliheshimu.

Wao wanawaza, wanawazia jambo lile lile leo hii. Hakika. Hili, "Tunajenga jengo kubwa. Tutakuwa na madhehebu makubwa. Tutajifanyia jengo lililo kubwa kuliko yote na watu waliovalia nadhifu kuliko wote, makasisi waliostaarabika kuliko wote." Wakati mwingine Mungu yuko umbali wa maili milioni kumi kutoka kwake. Hiyo ni kweli. Ingawaje, ni kanisa.

56 Kwa hiyo, kama Mungu anaheshimu tu ibada, uaminifu, dhabihu, Kaini alikuwa tu mwenye haki kama Habili. Lakini ilikuwa ni kwa ufunuo, ambapo yeye alielewa ya kwamba wazazi wake hawakula matofaa.

Nitasema jambo fulani hapa ambalo halionekani zuri kwa mhudumu, bali nitasema jambo hilo, haidhuru. Ninawasikia hawa wengine wakisema mambo, wakifanya mizaha midogo. Simaanishi jambo hilo. Nilisema hili, hata hivyo, "Kama kula matofaa kuliwafanya wanawake watambue kwamba walikuwa uchi, ni bora tusambaze matofaa tena." Unaona? Unaona? A-ha. Samahani kwa hilo, lakini ili kwamba tu libadilike. Nimewashikilia hapa, huku nikizungumza juu ya wanawake, na kadhalika. Na—na—nataka kuwatuliza kwa dakika moja, kwa ajili ya kile kinachofuata. Sasa, angalieni, ninyi. Haikuwa matofaa. Tunajua jambo hilo.

57 Kanisa limekuwa katika siku hizi, na mafanikio yake, kama mafanikio mengine yote yaliyobuniwa, linakuwa la kisayansi. Wanajaribu kutengeneza kanisa la kisayansi, la kuvutia kwa picha na minara mikuu. Na ni vibaya sana kwamba Wapentekoste waliingia katika mkondo huo. Mngelikuwa afadhali mkiwa na tari, kule pembeni, na Roho wa Mungu akiwazunguka. Lakini mnajaribu kujilinganisha na hao wengine, kwa sababu mmefanyika madhehebu. Hilo ndilo lililofanya jambo hilo. Mnaona? Makanisa yanajaribu kuwa ya kisayansi.

Na kumbukeni, wakati mwanadamu anapofanikiwa kwa njia ya sayansi, yeye anajiua mwenyewe kila siku. Wakati alipovumbua baruti, angalia kile ilichofanya. Wakati alipovumbua gari, linaua zaidi ya baruti inavyoua. Sasa yeye analo bomu la haidrojeni. Sijui atafanya nini na hilo? Sawa.

58 Na ndivyo ilivyo na kanisa, linapojaribu kufanikiwa kwa sayansi, kwa mpango wa kujibunia wa

mwanadamu, unakuondoa mbali zaidi na Mungu, na kuingia mautini, kuliko lilivyokuwa hapo mwanzo. Hiyo ni kweli. Usilichague kanisa lako jinsi ulivyomchagua mke wako. Unaona? Kile sayansi ilichomfanyia kilikuwa ni ajabu, bali ni bora ujiepushe na kanisa lako juu ya jambo hilo; alitengeneza rangi, poda, na vitu hivi vingine vyote. Chagua kwa tabia ya Neno Lake.

Sasa hebu tulinganishe bibi-arusi wa kawaida wa leo na anayejiita bibi-arusi wa kanisa wa siku leo. Linganisha mwanamke, atakayeolewa leo.

Sasa, angalia tu kile sayansi imemfanyia. Yeye anatoka, kwanza, akiwa amekata nywele zake, akiwa na moja ya nywele hizi za Jacqueline Kennedy, unaona, ama kitu kama hicho. Nanyi mnajua Biblia inasema nini? Biblia kwa kweli inampa mwanamume, kama akitaka, haki ya kumwacha kwa talaka, kama akifanya hivyo. "Yeye ni mwanamke mwenye sifa mbaya, ambaye atazikata nywele zake." Biblia ilisema hivyo. Sawa. Je! Hamkujua hilo? A-ha? Loo, naam! Ninahubiri sana California kwenu kutokujua hilo. Hiyo ni kweli. Loo, naam! Inanifaidia nini? Wanafanya hivyo, haidhuru. Huwezi kumchukua nguruwe na kubadilisha jina lake, kumfanya mwana-kondoo. Angalia.

59 Mtanichukia baada ya jambo hili, bali mtaijua Kweli. Unaona?

Angalia. Hebu tuvilinganishe. Huyu hapa anakuja amejaa rangi, kitu ambacho siye, bibi-arusi wa kisasa. Mnawishe uso wake, mume angelimtorroka, labda. Atakuogopesha vya kutosha, ukiondoa vitu hivyo vyote kwake. Na vivyo hivyo kanisa kubwa, liliopakwa rangi upande wa mbele, theolojia moto moto ya Max Factor. A-ha. Wote wawili wana u—uso mrembo, bandia, urembo uliobuniwa na mwanadamu na si urembo uliofanywa na Mungu. Hakuna tabia ya kutosha katika mmojawao.

Angalia, kama tu Shetani, ya kutosha kumdanganyia, mlinganishe bibi-arusi wa kisasa sasa na yeye: anavaa kaptura, anajipaka rangi, anakata nywele zake, anavaa nguo zinazofanana na za wanaume, na mkumsikiliza mchungaji aliyemwambia ya kwamba hayo yalikuwa sawa. Yeye ni mdanganyifu. Yeye atateseka kwa ajili ya hayo huko ng'ambo. Hiyo ni kweli. Anafanya hayo kudanganya, kuwa kitu asicho.

60 Hivyo ndivyo kanisa linavyofanya, wanapata DD ., Ph.D., LL.D. kubwa. Kwa hiyo mnasema, "Mchungaji wetu ni *hivi*, *vile*, na *vinginevyo*," Ihuenda hamjui Mungu zaidi Mhotentoti anavyojua kuhusu hekaya za Kimisri. Hiyo ni kweli. Sawa. Baadhi ya ujuzi wa seminari ya kitheolojia huko, na hawajui Mungu hata kidogo.

Kanisa la kisasa na rangi yao ya kitheolojia, wana wanawake wao wote ambao utukufu wao umenyolewa, na akina riki wao na mchungaji waliye naye, kama Yezebeli kama kulikuwako na mmoja. Nywele zilizokatwa, kaptura, rangi, vyote vimetengenezwa kwa ladha ya kitheolojia, hivyo ndivyo kanisa linavyosimama. Sawa. Lakini tabia yake ya kiroho iko mbali sana na kule kuwa mtunzaji nyumba ambaye Yesu Kristo anakuja kumpokea.

61 Kama Mkristo yeyote angemwoa mwanamke kama huyo, inaonyesha kuwa yeye ameanguka kutoka kwenye neema. Ladha yake ya Mungu na ladha yake ya makazi, jinsi makazi yanavyopaswa kuwa, iko mbali, anapomchagua mwanamke kama huyo. La, bwana. Hakika asingeridhisha ladha ya Mkristo. Tabia yake ya kiroho ni ya chini sana, imekufa, katika urembo wa kimadhehebu na tamaa ya ulimwengu.

Hapo ndipo hasa ambapo kanisa linasimama leo, liliuzhetani tabia yake liliyopewa na Neno, kwa ajili ya dini ya kisayansi ya kujibunia. Wakati, lilikuwa na haki, kama kanisa la Mungu, kudumu na Neno la Mungu na kuwa na Roho Mtakatifu akifanya kazi miongoni mwao, akiunganisha ule Mwili pamoja na Neno na upendo wa Mungu. Badala yake, likauza haki yake ya mzaliwa wa kwanza, kama Esau, na kuchukua dhehebu, ambalo lingemruhusu kutenda hayo, cho chote alichotaka, sawa, kusudi tu lipate kupendwa na watu kama mama yake alivyofanya huko Nikea Rumi. Neno la Mungu!

Loo, jinsi lilivyoingia katika milki yetu ya Kipentekoste! Ni vibaya sana, bali lilitendeka.

62 Angalia, kwa muda mfupi tu, mtawa katika kanisa Katoliki. Mwanamke huyo, ili kuwa mtawa, na anapochukua ule utaji wa mwisho, yeye amejitolea kabisa kwa kanisa hilo. Yeye ni (nafsi, mwili, na roho) mali ya kanisa hilo. Yeye hana nia yake mwenyewe. Hawezi kuwa nayo, wakati anapochukua utaji huo wa mwisho, hana nia yake mwenyewe, hana hiari yake mwenyewe. Angalia hapa nje, kwamba Shetani anawafanya walio wake wa uongo, kama walio wa kweli.

Kanisa la kweli la Kristo, Bibi-arusi, amejitolea sana Kwake na kwa Neno Lake lililoahidiwa, hadi nia ile ile iliyo ndani ya Kristo iko ndani yako. Ni tofauti ya jinsi gani!

Nasi tunaona leo hii, kwamba, kanisa la kisasa, kanisa la kisasa la ulimwengu. Lile kanisa la ulimwengu wa kisasa na pia kwamba lile Kanisa la kiroho yote mawili yamepata mimba, ili kuzaa wana.

Mmoja wao, uzazi wa kidhehebu, unafanyika, moja ya … siku, ili … siku hizi, kwenye Baraza la Makanisa Ulimwenguni, ambalo litauzalia ulimwengu yule mpinga-Kristo, kupitia dhehebu. Hiyo ni Kweli kabisa. Huenda nisiishi kuona jambo hilo. Naamini nitaliona. Lakini, ninyi vijana, kumbukeni ya kwamba

mlimsikia mhudumu akisema hivyo. Hilo hatimaye litamalizika. Na hiyo ndiyo alama ya mnyama, wakati anapounda hilo Baraza la Makanisa Ulimwenguni. Naye atamzaa mwanawe, yule mpinga-Kristo.

63 Lile lingine lina mimba kwa Neno la Mungu na litauzaa Mwili, ule Mwili uliokamilika wa Yesu Kristo, ambao ni Bibi-arusi. Mwili wa Kristo haujakamilika bado. Ni wangapi wanaojua jambo hilo? Mwanamume na mwanamke ni mmoja. Naye Kristo ni Mwili mmoja, Neno. Bibi-arusi atapaswa kuwa sehemu ya Mwili huo uliosalia. Na hao wawili, pamoja, wanaufanya huo Mwili mmoja tena. Kama vile Adamu alivyokuwa hapo mwanzo: mwanamume, mkewe, ni mmoja. Sasa, Yeye, yule Bibi-arusi wa kweli, amejitolea sana Kwake, hata hatumii nia Yake mwenyewe tena. Nia Yake, bila shaka, ni mapenzi Yake, na mapenzi Yake ni Neno Lake.

64 Sasa mwangalie huyu anayeitwa bibi-arusi aliyechaguliwa na mwanadamu, na ulinganishe wa kiroho na wa kawaida wa leo hii, Yezebeli wa kisasa aliyerogwa na Ahabu wake, urembo wa Max Factor, kila kitu. Liangalie kanisa, vivyo hivyo, bali ni malaya kwa Neno la Mungu aliye hai; madhehebu makubwa, majengo makubwa, fedha nyingi, mshahara mkubwa, yote yamejiuza. Watu wakisimama mimbarani wakiidhinisha ya kwamba hayo ni sawa, na kuwaacha waendelee nayo. Ni udanganyifu tu, hivyo tu. Kweli ni wakati wa Kanisa la Laodikia lililo kipofu, jinsi hasa Biblia ilivyosema lingekuwa. "Likasema, 'Mimi ni tajiri. Nimeketi kama malkia. Sina haja ya kitu.' Nawe hujui ya kuwa wewe ni maskini, mwenye mashaka, kipofu, mnyonge, uchi; nawe hujui." Kama hiyo si BWANA ASEMA HIVI, Ufunuo 3, sijaisoma kamwe. Hivyo ndivyo alivyo, wala hajui! Wazia jambo hilo.

65 Kama ungemwambia mwanamume ama mwanamke, barabarani, ambaye alikuwa uchi kabisa, na kuwaambia walikuwa uchi, nao wanasema, "Shika lako," mbona, kuna upungufu wa akili hapo mahali fulani. Kuna shida fulani ya akili zao.

Na wakati unapoweza kusoma Neno la Mungu, jinsi watu wanavyopaswa kufanya, na huu ubatizo wa Roho Mtakatifu tulio nao leo hii, na, watu, mbona, wanakuangalia kana kwamba ulikuwa mwendawazimu. Unawaambia: "Mnapaswa …" Hawana budi kuzaliwa mara ya pili. Hawana budi kuamini Biblia.

66 Wao wanasema, "Hiyo ilikuwa ni hadithi ya Kiyahudi, kwa miaka mingi iliyopita. Kanisa letu linayo njia." Wanyonge, wenye mashaka, vipofu, uchi, na hata hawajui. Ni ninii … Na Biblia ilisema ya kwamba hiyo ndiyo hali wanayofikia.

Ingewezekanaje nabii wa kweli kukosa kuona jhayo? Sijui.

Inaingia moja kwa moja katika makanisa yetu yote, kila mahali. Iangalie tu, katika mwelekeo wa kisasa. "Yule kahaba wa kale na binti zake," wa Ufunuo 17, akiwapa wale watu "maskini, vipofu, wenye mashaka" mafundisho yake ya theolojia kinyume na Neno la Mungu. "Nao walipata ndani yake nafsi za watumwa, na wanaume na wanawake wa—wa kila mahali." Badala ya kuwavutia watu …

Kristo hulithibitisha Neno Lake, ambalo huvutia watu. Yeye hawavutii watu kwenye makanisa ambao wanavutiwa na madhehebu makubwa na matamasha makuu, na mambo makuu yasiyofaa pamoja na vitu vya kuvutia macho. BaliNeno la Mungu linamvutia Bibi-arusi wa Kristo.

67 Sasa tazama. Inapendeza ku—kuona jinsi ambavyo—ambavyo kanisa linajaribu kuvutia usikivu wa watu kwa njia ya majoho mazuri na kwaya zilizovalia rasmi, na wanawake waliokata nywele zao na nyuso zilizopakwa rangi. Nao wanafikiri … Nayo iliimba kama Malaika. Wakadanganya kama ibilisi, wakizurura-zurura usiku kucha kwenye dansi kama, pasipo kuwaza lolote kuhusu hilo. Na hivyo ndivyo wanavyowazia, "Ni sawa. Hayo ni mazuri." Lakini, unaona, hayo ni ya bandia. Hayo si Neno la Mungu.

68 Huku, Bibi-arusi wa kweli huvutia macho ya Mungu, kwa kulishika Neno Lake. Sasa angalia. Sasa hebu na tumwangalie Kristo.

Unasema, "Vema, sasa, ngoja kidogo, vipi kuhusu uzuri huu unaonena habari zake?"

Biblia ilisema, katika Isaya 53:2, ya kwamba, wakati Yesu alipokuja, "Hakukuwako na uzuri juu Yake, kwamba tungemtamani Yeye." Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Hana uzuri. Kama angalikuja katika uzuri wa kilimwengu, kama Shetani alivyo leo, watu wangelimkimbilia na kumkubali jinsi wanavyolifanya kanisa leo hii. Wangalimwamini Yeye, wangempokea, kama wanavyomfanyia Shetani leo hii. Hakika, wangefanya hivyo. Lakini Yeye hakuja katika uzuri wa aina hiyo, bali daima Yeye huja katika uzuri wa tabia. Hapo, Kristo hakuwa Mtu mzuri, mkubwa, mwenye nguvu, mnene. Mungu hachagui watu wa aina hiyo.

69 Ninakumbuka wakati mmoja nabii alikwenda ku—kuchagua mfalme, kumfanya mwana wa Yese mfalme, akachukue mahali pa mfalme mwingine, Sauli. Na kwa hiyo Yese akamleta, mvulana wake mkuu, mkubwa, mzuri. Yeye akasema, "Taji itaonekana sawa, kichwani mwake."

Nabii alienda kummiminia mafuta. Akasema, "Mungu amemkataa." Naye akamkataa kila mmoja wao, hata alipomfikia maskini jamaa mdogo mwenye mabega yaliyoinama, mwekundu. Naye akammiminia yale

mafuta, na kusema, "Mungu alimchagua huyu." Unaona? Sisi huchagua kwa macho. Mungu huchagua kwa tabia.

Tabia, hapajakuwako na tabia kama ya Yesu Kristo. Inaishi ndani yako na kumdhihirisha Yeye. Tunaona hiyo ni kweli. Si uzuri Wake wa kilimwengu unaomvutia Bibi-arusi Wake. Ni tabia Yake, tabia ya Kanisa, ambayo Yesu anatafuta; si mahali palipo na majengo makubwa, ambapo pana madhehebu makubwa, ambapo pana washirika wengi. Yeye aliahidi kukutana nao mahali popote ambapo wawili watatu wamekusanyika pamoja. Kweli. Hapo ndipo mwaminio wa kweli anapoweka matumaini yake, ni juu ya hilo Neno la Mungu likithibitishwa katika Kweli, ilivyo. Walichaguliwa kwa Neno Lake, si kundi linalopenda ulimwengu. Wanauchukia huo.

Si ajabu hilo limetalikiwa na Yeye, kwa sababu limeukosa ufunuo Wake, wala halina. Yeye halijali, jinsi linavyotenda na kufanya, na ni kiasi gani cha mambo haya ya kilimwengu lilicho nacho.

70 Anatafuta tabia yake, ile tabia ya Kristo. Sasa, hebu kidogo tu sasa. Hivyo ndivyo ilivyo. Yeye huchagua Bibi-arusi ili aakisi tabia Yake, ambapo makanisa ya kisasa ya leo hakika yanakosa mpango Wake—Wake hapa, maili milioni moja, kwa sababu wao wanakana *Hili* kuwa ile Kweli. Kwa hiyo ingewezekanaje? Sasa, Yeye anatazamia siku ambayo Bibi-arusi huyo ataumbika, Waebrania 13:8, kama tu vile ilivyokuwa, jinsi Yeye alivyokuwa. Haina budi kuwa ni mwili Wake ule ule, mifupa ile ile, Roho yule yule, kila kitu kile kile, kujengeka vile vile kabisa, na hao wawili basi wanakuwa mmoja. Hadi kanisa litakapokuwa hivyo, bado hawajawa mmoja. Tabia Yake, lile Neno, kwa ajili ya wakati huu, halina budi kufinyangwa. Bibi-arusi hana budi kufinyangwa kama Yeye alivyo.

71 Sasa, katika kufunga, nataka kusema sababu ya mimi kusema mambo haya, nami nita—nitafunga. Hivi majuzi usiku, yapata saa tisa alfajiri, niliamshwa.

Nataka yeyote wenu kujibu hili. Je! Nimewahi kuwaambia jambo lo lote katika Jina la Bwana ila lile lililokuwa sahihi? Daima imekuwa sahihi. [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Kwa hiyo anisaidie, Mungu anajua hiyo ni kweli. Hakuna chochote, mahali po pote ulimwenguni, katika maelfu ya mambo ambayo yamesemwa, ambayo Yeye alikosa hata kwa neno moja lake. Daima limetimia kikamilifu.

Hata ilipokuwa Phoenix, hivi majuzi, ama yapata mwaka mmoja uliopita, na nikawaambia juu ya Ujumbe huo wa—juu ya *Ni Wakati Gani, Mabwana?* Na nikawaambia, "Malaika Saba wangekutana huko," na ingekuwa ni kule kufunguliwa kwa Mihuri hii, na chochote kile. Na hapo gazeti la—la *Life* lilichapisha makala juu yake, Mwali huu mkuu uliopaa hewani, maili thelathini kwenda juu, upana wa maili ishirini na saba. Wakasema hawakujua ilikuwa ni nini; hawajui bado. Na watu wanaoketi papa hapa katika jengo hili usiku huu, walikuwa wamesimama papo hapo pamoja nami wakati lilipotukia, vile vile hasa ilivyosema. Yeye aliniambia mambo yatakayokuja kutimia, na yalitukia vile hasa. Jinsi ambavyo kila moja ya ile Mihuri ilivyofunguliwa, na kueleza mafumbo yaliyokuwa yamefichwa kotekote kwenye zile nyakati hizo za watengenezaji na kadhalika, kikamilifu kabisa.

72 Jinsi ambavyo, wakiwa wamesimama juu ya kilima, wanaume, watatu ama wanne wakiwa wamesimama humu humu sasa, naam, zaidi ya hao. Nilipokwa nikipanda hicho kilima, Roho Mtakatifu akasema, "Twaa lile jiwe." Tulikuwa tukiwinda. Akasema, "Itupe juu hewani, na useme, 'BWANA ASEMA HIVI.'" Nilifanya hivyo. Kutoka chini kule kukaja upepo mdogo wa kisulisuli. Nikasema, "Katika muda wa saa ishirini na nne, mtaona mkono wa Mungu." Watu walioketi papa hapa sasa.

Kesho yake, yapata saa nne, tukiwa tumesimama pale, nikasema, "Iweni tayari. Ingieni chini ya gari pale," mzee mzoefu. Nikasema, "Jambo fulani linakaribia kutukia." Anga lilikuwa angavu, moja kwa moja katika genge kubwa. Moto wa kisulisuli ukashuka kutoka Mbinguni, wenye sauti kuu sana uwezavyo kuwa na sauti, ukazigonga kuta namna hiyo. Ni—nilikuwa nimesimama moja kwa moja chini Yake. Nikavua kofia yangu, nikashika kichwa changu. Ukaja yapata kama futi tatu au futi nne juu yangu, na kuchimba shimo kote kuzunguka ule ukuta hivyo namna hiyo, na ukalipuka. Ndipo ukarudi juu hewani, na kuzunguka-zunguka tena, na kushuka chini, mara tatu, hata ulikuwa umekata vilele vya vichaka vya mesketi kule, umbali wa yadi mia mbili. Mnawasikia jamaa hao wakisema, "Amina"? Walikuwa kule wakati jambo hilo lilipotukia, unaona, na kulipuka mara tatu.

73 Walipotoka chini ya yale magari na kila kitu, wakarudi kule, wakasema, "Hilo lingekupiga, usingesalia hata doa."

Nikasema, "Ilikuwa—Ilikuwa ni Yeye. Alikuwa akizungumza na mimi." Mungu hunena kwa upepo wa kisulisuli. Unaona? Na kulikuweko na Nguzo ile ile ya Moto mnayoiona kwenye picha, ikiwa imesimama pale.

Na wakati ilipopanda juu, wao wakasema, "Ni kitu gani?"

Nikasema, "Hukumu inaipiga Pwani ya Magharibi."

Siku ya pili kutokea hapo, Alaska nusura izame. Unaona? Ukapiga mara moja, pale, pigo la kwanza.

Ambapo, huna budi kufanya jambo fulani, kuiainisha. Kama vile yule mtu aliyetia chumvi kwenye chupa, na kuitupa majini, na kusema, "BWANA ASEMA HIVI, na kuwe na maji matamu." Na mwingine, Yesu alichukua maji na kuyamimina katika mtungi, na—na kutengeneza divai kwayo.

Huna budi kuwa na kitu fulani, kuiainisha. Hicho ndicho hilo lilkuwa, hilo lililotupwa juu hewani na kurudi chini. Hilo lilianzisha kile kisulisuli kidogo. Katika muda wa saa ishirini na nne, ulikuwa umeutikisa huo mlima mpaka ukachimba mtaro kuuzunguka.

74 Kasisi Bw. Blair anayeketi hapa, ninamwangalia moja kwa moja sasa, alikuwa kule juu na akachukua baadhi ya vipande vyake, na kadhalika. Huyu hapa Terry Sothmann, hao, na wakiwa wamesimama hapa, na Billy Paul. Na ndugu, baadhi ya wengi wa hawa wengine wanaoketi hapa ndani, ambao walikuwa papo hapo kuona jambo hilo likitukia wakati ulipoupasua.

Hiyo si hadithi ya kubuni. Hiyo ni kweli. Hilo halikuwa huko nyuma katika siku za Biblia. Hiyo ni sasa. Unaona? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Mungu yeye yule ambaye daima alinionyesha mambo haya, nayo yametimia, kikamilifu kabisa. Kamwe hayajashindwa hata wakati mmoja. Sasa ninamjivunia Yeye.

75 Wiki chache zilizopita, nilikuwa katika ono. Nami nilikuwa nimesimama juu ya—kwenye mahali pa juu, nami nilikuwa nione mwoneko wa Kanisa. Nami nikaona, likija kutokea kwenye ninii wangu … Nilikuwa nimesimama *hivi*, nikielekea Magharibi. Na upande *huu* kulikuja kundi la wanawake wazuri sana, waliovalia vazi zuri hasa, nywele ndefu zilizotengenezwa vizuri kwa nyuma, nguo zenye mikono mirefu, na sketi ndefu nadhifu. Nao wote walikuwa wakipiga hatua taratibu, kama, "Twendeni, askari Wakristo, tukitembea kama waendao vitani, na msalaba wa Yesu ukitangulia." Na walipokuwa wakipita, nilisimama, na kulikuwa na Kitu fulani pale, Roho fulani, alikuwa ni Mungu, na kusema, "Huyo hapo Bibi-arusi." Nami nikaangalia, na moyo wangu ulikuwa na furaha. Naye akazunguka upande *huu*, kisha akapita nyuma yangu.

Baada ya kitambo kidogo, huyu bibi-arusi aliporudi *huku*, Ikasema, "Sasa kanisa la kisasa litaonekana kimbele." Na hili hapa kanisa la Asia likaja. Sijapata kuona kundi uchafu kama hilo.

Haya hapa yale makanisa mengine yakija, ya mataifa mbalimbali. Walionekana wa kutisha.

76 Nami na—nasema jambo hili kwa sababu nina wajibu wa kusema ukweli, mbele za Mungu. Na Yeye aliposema, "Hili hapa kanisa la Marekani linakuja sasa, likaonekane kimbele." Kama niliwahi kuona kundi la mashetani, lilikuwa hilo. Hao wanawake walikuwa uchi, wakiwa na kitu cha kale kama cha rangi ya kijivu, kama rangi ya ngozi ya tembo. Nao walikuwa wamekishikilia mbele zao, pasipokuwa na sehemu yake ya juu hata kidogo. Nao walikuwa wakifanya upuuzi wa namna hii, ambao, hizi—hizi dansi ambazo hawa vijana hucheza hapa, kule kujisokota na mengineyo, na aina hiyo ya muziki ukiendelea. Na nilipomwona Bibi Amerika. amejitokeza, nusura nizimie.

Sasa, hii ni BWANA ASEMA HIVI. Kama mnaniamini mimi kuwa mtumishi Wake, niaminini sasa. Nisingesema jambo hilo bure kamwe. Hakuna fedha za kutosha ulimwenguni kote kunifanya niseme mambo hayo kama hayangalikuwa kweli.

Na wakati alipopita huko, hicho kilikuwa kitu kilichoonekana kichafu sana nilichowahi kuona. Nikawazia, "Mungu, jinsi wahubiri na sisi ndugu tumejitahidi kukutafutia Wewe Bibi-arusi, na hilo ndilo bora tuliloweza kufanya." Alikuwa akijisokota, akiwa ameshikilia *hiki* mbele yake, kama moja ya sketi hizi za dansi, akikishikilia mbele ya sehemu yake ya chini, sehemu yake ya chini, namna *hii*, huku akicheza dansi na kujisokota kama watoto hawa wanavyofanya hapa kwenye … kwenye maonyesho haya machafu waliyo nayo, kujisokota. Huyo alikuwa ni Bi. Ukristo wa Marekani.

77 Hivyo nisaidie, kwa msaada wa Mungu, hivyo ndivyo linavyoonekana machoni Pake. Ni—nilininii tu … Nikaanza … Ningeweza kuzimia. Nikawaza, "Kujaribu kote, na kuhubiri, na kushawishi?" Kila mmoja wao akiwa na nywele zilizokatwa, nao walikuwa wakijisokota na kufanya yasiyofaa, wakishikilia *hiki* mbele zao. Wakaja pale, mahali nilikokuwa nimesimama pamoja na hiki Kiumbe cha kimbinguni. Nisingeweza kumwona Yeye. Ningemsikia Yeye akizungumza nami; alikuwa karibu na mimi. Lakini walipogeukia upande *huu*, wanashikilia *hiki*. Na huku wakijisokota tu na kucheka na kuendelea, wakiendelea namna hiyo, wakishikilia *hiki* mbele yao.

Sasa, mimi nikiwa nimrsimama Uweponi Mwake pale, nikiwa mtumishi Wake. "Na kwa yote yale niliyojaribu, hayo ndiyo bora sana niliyoweza kufanya?" Nikawaza, "Mungu, ilinifaidi nini? Ilifaidi nini? Kulia kwote, na kusihi, na kushawishi, na zile ishara kuu na maajabu na miujiza ambayo Wewe ulionyesha. Na jinsi nilivyosimama pale, na kwenda nyumbani na kulia baada ya kuwahubiria hao na kadhalika, nayo ilinifaidi nini? Na halafu inanibidi kukukabidhi Wewe kitu kama hicho, kama Bibi-arusi?"

78 Na nilipokuwa nimesimama pale, nikiangalia, huyo bibi-arusi akapita. Nawe unaweza kuwazia sehemu yake ya nyuma, hamna kitu, akishikilia *hiki* mbele yake wakati akiendelea kujikokota huku akicheza dansi, namna hiyo, kujisokota, akirusharusha viungo vyake namna hiyo. Na, yeye, loo, ilikuwa ni chafu, jinsi

alivyokuwa akijiendesha, mwili wake ukitikiswa namna hiyo. Sasa mimi …

Unasema, "Inamaanisha nini, Ndugu Branham?" Sijui. Ninawaambia tu yale niliyoona.

Na wakati huyo alipopita namna hiyo, nikamwangalia. Loo, nikawa dhaifu kabisa. Niligeukia tu upande mwingine. Nikawaza, "Mungu, nimehukumiwa. Hakuna—hakuna haja ya mimi kujaribu lolote sasa. Afadhali tu niache."

Bibi Carl Williams, kama umeketi hapa, na ile ndoto uliyonisimulia, muda mfupi uliopita, uliyokuwa nayo hivi majuzi, ambayo imekuwa ikikusumbua, hiyo hapo. Usukani umeondolewa mkononi mwangu.

79 Ndipo, nikawaza tu, "Ni—ni afadhali nisahau hayo." Nilikuwa nimekwisha.

Ndipo, mara, nikasikia Hilo likija tena. Na upande *huu* akaja Bibi-arusi yule yule aliyekwenda upande *huu*. Hawa hapa wale wasichana wadogo wanakuja tena, na kila mmoja wao alikuwa amevalia vazi lao la kitaifa walikotoka, kama vile Uswisi, Ujerumani, na kwingineko, kila mmoja amevalia vazi la namna hiyo, wote wanazo nywele ndefu, kama vile wale wa mwanzoni. Nao hawa hapa walikuwa wakija, wakitembea. "Twendeni, askari Wakikristo, kama waendao vitani." Na wakati wote walipopita kwenye kituo cha kukaguliwa kwanza ambapo tulikuwa tumesimama, mara, kila jicho likaelekea upande ule. Na kisha wakageuka, nao wakaendelea, wakitemeba kwa utaratibu.

Na mara walipoanza kwenda moja kwa moja angani, huyu mwingine akapanda kwenye kilele cha kilima kutelemka, namna *hiyo*.

Hawa wakaanza kupiga hatua moja kwa moja hata angani. Na wakati walipoanza kupiga hatua, niliona wasichana kadha wadogo huko nyuma, walionekana kama huenda wakawa ni wasichana wa kigeni, kama Waswideni au Waswisi, ama mahali fulani. Wakaanza kuangalia huku na huko, na ku-... Nikasema, "Msifanye hivyo! Msiache hizo hatua!" Na nilipopaza sauti namna hiyo, nikaja, katika lile ono, nikiwa nimesimama pale huku nimetoa mkono wangu namna *hiyo*. Nikawaza, "Vema …"

80 Hiyo ndiyo sababu nilisema yale niliyo nayo, usiku wa leo. Nataka kuwaulizeni swali. Je! Imechelewa kuliko tunavyowazia? Je! Huenda ikawa tayari ameitwa na kuchaguliwa, akatiwa muhuri? Hakutakuwako na mmoja zaidi, mwajua. Je, inawezekana? Loo, naam. Loo, naam.

Kumbukeni yale niliyosema, hivi majuzi kwenye kiamshakinywa. Katika chavua ya kuzalisha ya kiume na ya kike, kuna chembechembe hai milioni moja ambazo hutokea, mayai milioni moja hutoka. Lakini kuna moja tu ya hiyo inayoishi, na, hata hivyo, kila mmoja anafanana tu: mmoja kati ya milioni moja. Kila moja ya hayo, ni yai lile lile na mbegu ile ile. Moja yao huishi. Hizo nyingine hufa.

Hakuna mtu anayeweza kusema ni lipi kati ya mayai hayo lililo tayari, na, loo, lolote kulihusu hilo. Mungu hana budi kuamua jambo hilo, kama itakuwa ni mvulana ama msichana, mweusi au mwenye nywele za rangi ya shaba ama nyeusi, ama cho chote kile itakachokuwa. Mungu huamua hayo. Si ile ya kwanza kukutana, bali lile ya kwanza ambayo Mungu ameamua. Labda mmoja inakuja *hapa* juu, na mmoja … Kama uliwahi kuona, katika ile chupa ya majaribio, kuona zikija pamoja. Nimeziangalia. Mungu hana budi kuamua hayo. Mmoja, kila moja ya hizo, zinafanana tu, bali kwa kuteuliwa. Kuzaliwa kwa kawaida ni kwa kuchaguliwa. Mungu humchukua mmoja katika milioni.

81 Wakati Israeli walipoondoka Misri, wakielekea kwenye nchi ya ahadi, walikuwa kadiri ya watu milioni mbili. Kila mmoja wao alikuwa chini ya mwana-kondoo yule yule wa sadaka, la sivyo wasingeishi. Kila mmoja wao alimsikiliza Musa, nabii. Kila mmoja wao alibatizwa kwake, katika Bahari ya Shamu. Kila mmoja wao alicheza, wale wanawake pamoja na Miriamu, huku na huko kando ya (ambapoi) ufukwe wa bahari, wakati Mungu alipomwangamiza yule adui. Kila mmoja wao alisimama pamoja na Musa, na kumsikia akiimba katika Roho. Wao, kila mmoja, walikula mana jangwani, ambayo ilishuka kutoka Mbinguni. Mana mpya, kila usiku, ambao ni mfano wa Ujumbe, kila mmoja wao alikula hiyo. Lakini, kati ya hao milioni mbili, ni wangapi waliofanikiwa? Wawili. Mmoja kati ya milioni moja.

Kuna karibu Wakristo milioni mia tano ulimwenguni usiku wa leo, tukiwahesabu Wakatoliki na wote. Milioni mia tano ya wanaojiita waaminio ulimwenguni. Kama Unyakuo ungekuja usiku wa leo, hilo lingemaanisha … kama hesabu ingekuwa mmoja kati ya milioni moja. Sisemi ndivyo ilivyo. Lakini kama ingekuwa hivyo, watu mia tano, katika muda wa saa ishirini na nne zijazo, wangekosekana. Hata usingelisikia habari zake kamwe. Kutakuwako na kama hao watakaokosekana, hata hivyo, ambao hata hawangejulikana waliko.

82 Ndipo ingewezekana, kutendeka kwetu, ewe rafiki, kama ilivyokuwa wakati Yohana Mbatizaji alipokuja. Hata wanafunzi walisema, "Mbona Maandiko yalisema, mbona mi—mitume ama manabii wanasema, mbona inasema kwamba Eliya hana budi kuja kwanza na kurejesha mambo yote?"

Yeye akasema, "Nawaambieni ya kwamba Eliya amekwisha kuja, nanyi hamkutambua hilo."

Moja ya siku hizi tungeweza kuachwa tukiwa tumeketi hapa, "Vipi kuhusu Unyakuo kabla ile dhiki

haijaanza?"

"Tayari umekwishakuja na hamkujua hilo."

83 Mwili wote, umetiwa muhuri, unapiga tu hatua. Sisemi kwamba hivyo ndivyo ilivyo. Natumaini sivyo ilivyo. Lakini, ewe rafiki, inapoachilia …

Kama tunajisikia moyoni mwetu, usiku huu, ya kwamba tunapaswa kuyanyoosha maisha yetu, na mambo ambayo tumefanya, hebu niwashauri, kama ndugu mhudumu. Nitasema jambo hili kwa mara yangu ya kwanza, mimbarani. Nimevuta kidogo zaidi usiku huu, juu ya *Huu*, kuliko nilivyowahi kufanya juu ya kitu kingine chochote, wakati wo wote, vyovyote, hadharani, kwa sababu nimekuwa na uhuru mkuu katika mikutano hii. Kama mnaniamini mimi kuwa nabii wa Mungu, sikilizeni yale niliyowaambia. Kama kuna hata mlio mdogo tu wa hisia moyoni mwako, wewe mwendee Mungu sasa hivi. Ufanye hivyo.

84 Simameni kidogo, enyi watu. Angalia kanuni za—zako za imani unazozitumikia. Angalieni katika makanisa yenu. Je! Yanaambatana kabisa na Neno la Mungu? Je! Umetimiza kila sharti? Unasema, "Mimi ni mtu mzuri." Vivyo hivyo na Nikodemo, na vivyo hivyo wengine wote. Wao—wao walikuwa wazuri. Unaona? Hilo halina uhusiano wowote na Hilo.

Na, enyi wanawake, nawatakeni mwangalie kwenye kioo, na mwangalie yale Mungu anayomtaka mwanamke kufanya. Na utazame katika kioo cha Mungu, si katika kioo cha kanisa lako sasa, katika kioo cha Mungu; na uone kama ungeweza kuhitimu, maishani mwako, Bibi-arusi wa kiroho wa Yesu Kristo.

Wahudumu, wazeni vivyo hivyo. Je! Mnakata kona *hapa*, kusudi usimuudhi mtu fulani humo? Je, ungefanya jambo *hili* kama haikuwa … nao watakufukuza kanisani? Kama unajisikia hivyo, ndugu yangu mpendwa, hebu nikuonye, katika Jina la Yesu Kristo, likimbie hilo sasa hivi.

Na, ewe bibiye, kama huwezi kutimiza masharti ya Mkristo, si kama Mkristo wa kawaida; bali moyoni mwako, na maisha yako yanalingana kabisa na hati ya ndoa ya Mungu hapa inavyosema inabidi iwe hivyo.

Na, mshiriki wa kanisa, kama kanisa lako haliko hivyo, halitimizi masharti ya Mungu ya Neno Lake, ondoka humo na uingie katika Kristo.

85 Hilo ni onyo zito. Hatujui ni wakati gani, nanyi hamjui ni wakati gani, ambapo mji huu siku moja utakuwa umezama humu chini ya bahari hii.

"Loo, Kapernaumu," Yesu akasema, "ewe uliyeinuliwa mpaka mbinguni, utashushwa mpaka kuzimu. Kwa kuwa, kama zile kazi kuu zingefanywa katika Sodoma na Gomora, ingalikuwako hata leo." Na Sodoma, Gomora imezama chini ya Bahari ya Chumvi. Na Kapernaumu uko chini ya bahari.

Ewe mji, unayejidai kuwa mji wa Malaika, ambao umejiinua mpaka mbinguni, na kupeleka mambo yote machafu, mambo machafu ya mitindo na kadhalika, mpaka hata nchi za ng'ambo zinakuja hapa kuchukua uchafu wetu na kuupeleka mbali, kwenye makanisa yako mazuri na minara, na kadhalika, jinsi mnavyofanya. Kumbkai, siku moja utazama chini ya bahari, masega yako makuu yakiwa chini yako sasa hivi. Ghadhabu ya Mungu inakokomoa papa hapa chini yako. Ni muda gani zaidi atazuia ufukwe huu unaoning'inia kule? Wakati, bahari hiyo huko ng'ambo, yenye kina cha maili moja, itatelezea mle, moja kwa moja hadi kwenye Bahari ya Salton. Itakuwa mbaya zaidi kuliko ile siku ya mwisho ya Pompeii. Tubu, Los Angeles.

Tubuni, ninyi wengine, mkamrudie Mungu. Ile saa ya ghadhabu Yake iko juu ya nchi. Kimbieni wakati kukiwa na wakati wa kukimbia, na mwingie ndani ya Kristo.

Hebu na tuombe.

86 Mungu mpenzi, huku, katika roho yangu, ninatetemeka, moyo wangu unadondosha machozi ya maonyo. Tujalie, Ee Mungu, ya kwamba wanaume na wanawake hawatachukulia yale niliyosema kama mzaha, na watu wa kanisa hawatawazia jambo hilo kama kitu ambacho cha maonevu au kuwapinga. Jalia waone, Bwana, ni katika upendo.

Wewe unanishuhudia, Mwenyenzi Mungu, kwamba nimeenda huku na huko kwenye pwani hii, mwaka baada ya mwaka, nikitangaza Neno Lako. Nishuhudie, Ee Mungu, kama ingelitendeka usiku wa leo, nimesema Kweli. Wewe unajua ono hili la Bibi-arusi ni Kweli. Nimechukua Jina Lako kwa njia ya hilo, Bwana, na kusema ilikuwa ni BWANA ASEMA HIVI. Nami ninajisikia ya kwamba ninajua, Bwana, juu ya yale ninayofanya.

Kwa hiyo ninakuomba Wewe, Bwana, katika Jina la Yesu, hebu watu wajitikise, usiku wa leo, na kuikimbia ghadhabu inayokuja, kwa maana Ikabodi imeandikwa milangoni na juu ya mataifa. Alama nyeusi ya kukataliwa imetiwa kwake. Roho wa Mungu amehuzunishwa akaondoka kwake, nao wamepimwa katika mizani na kuonekana wamepungukiwa. Ile karamu ya Mfalme Nebukadreza imejirudia tena, pamoja na

karamu za walevi na wanawake walio nusu uchi, wakijiita Wakristo.

87 Ee Mungu wa Mbinguni, hurumia ulimwengu wenye dhambi na watu wenye dhambi, Bwana, kama tulivyo usiku wa leo. Mungu, ninajaribu kusimama katika pengo na kuomba rehema ya Kiungu, ya kwamba utanena na umati huu usiku wa leo na kumhamasisha Bibi-arusi Wako, Bwana, apige hatua taratibu si kwa ishara ya kanuni yoyote ya imani, bali kwa sauti ya Injili ya Bwana Yesu Kristo. Tujalie, Ee Mungu. Hebu ijulikane, usiku huu, ya kwamba Wewe ni Mungu, na Neno Lako ni Kweli. Huku, kwa uchaji, mbele ya macho ya watu hawa, tunawahamasisha Neno Lako.

Katika Jina la Yesu Kristo, ninawaombea, Bwana. Wamekuona Wewe, bila shaka yo yote, ukitembea kwenye umati wao na kuwaambia yaliyo moyoni mwao. Nawe unajua, Bwana, yale, yanayoendelea, sasa hivi. Wewe unajua hiyo ni Kweli, Ee Mungu. Nami nakuomba, katika Jina la Yesu, jalia Roho Mtakatifu atuombee tena, Bwana, na avute kutoka kwa wasikilizaji hawa, Bwana, wale walioandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo. Tujalie, Ee Mungu. Ninaomba kwa moyo wangu wote.

Watu hawa, kwa kawaida, Bwana, wangenipa senti ya mwisho waliyokuwa nayo, kuunga mkono Ujumbe. Wangefanya chochote wangeweza. Lakini, Ee Mungu, inapofikia kuambatana Nao, na kuingia ndani Yake, naomba, Mungu, ya kwamba huu utakuwa ndio usiku ambao utawapa thawabu na kumwaga Roho Wako Mtakatifu juu ya mkutano huu. Na jalia kusiwe na mchezo au kurukaruka huku na huko, bali kuomboleza na kulia, na kutubu, wakishikilia pembe za madhabahu, tunapoona hukumu zikija chini yetu, usiku wa leo. Tujalie hilo, Mungu. Ninaomba kwa uaminifu nijuavyo, katika Jina la Yesu Kristo.

88 Ndugu yangu, dada, si—sijui niseme nini zaidi, kama nimepata neema machoni penu, kwa uweza wa Mungu, kama unaniamini mimi kuwa nabii Wake. Hii ndiyo mara ya kwanza kusema hilo hadharani. Lakini nasikia onyo la ajabu la namna fulani. Mimi sizoelei hili. Mnajua sizoelei. Mimi sitendi namna hii. Nilisita kunena huo Ujumbe na kusema mambo hayo. Niliyakwepa na kadhalika, nisije nikafanya hivyo. Lakini yamekwishakusemwa, nayo yatasimama kwenye ile Siku ya Hukumu, kama ushuhuda ya kwamba nimesema Kweli. Hiyo ni BWANA MUNGU ASEMA HIVI! …?…

Loo, enyi Pentekoste, kimbieni kwa ajili ya maisha yako. Kimbilieni zile pembe za madhabahu na mlie, kabla haijachelewa sana, kwa kuwa saa itakuja ambapo mnaweza kulia na haitafaa kitu. Kwa kuwa Esau alitafuta apate mahali, pa haki yake ya mzaliwa wa kwanza, na hakuweza kuipata. Nakukabidhi, ewe, California. Enyi, mkutano wa Wafanyabiashara wa Injili Yote, ambao nawapenda, ambao nimewaacha na kuwakumbatia, kwa moyo wangu wote, nawakabidhi kwa Yesu Kristo, usiku wa leo. Mkimbilieni Yeye! Msimruhusu Ibilisi awapoze mbali na Hili. Dumuni moja kwa moja Nalo hata mtakapokuwa, kila mmoja, mmejazwa na Roho Mtakatifu, sana, hata itawafanya mje kwenye Neno hili, litakalowafanya ninyi wanawake kujitengeneza, litakalowafanya ninyi wanaume mjitengeneze. Kama ukisema unaye Roho Mtakatifu, huku huwezi kuambatana na Neno, ni roho mwingine aliye ndani yako. Roho wa Mungu yuko kwenye Neno Lake, Umasihi, Neno lililopakwa mafuta. Bibi-arusi hana budi kuwa Masihi mdogo, Neno lililopakwa mafuta.

89 Hebu tusimame kwa miguu yetu, katika Jina la Bwana Yesu Kristo. Kama hamtaisikia sauti yangu tena … Lakini, Mungu akipenda, ninaondoka kwenda Afrika, katika muda wa saa chache. Huenda nisirudi kamwe. Sijui. Lakini nawaambia, kwa moyo wangu wote, nimewaambia Kweli. Sijaepuka kuwatangazia kila kitu ambacho Mungu ameniambia niseme. Nami nimesema jambo Hilo katika Jina la Bwana.

Ni wakati wa uchaji mno. Sijui jinsi ya kulielezea. Nimejaribu kuondoka mimbarani mara tatu ama nne, nami sikuweza kufanya hivyo. Hii ni saa ya uchaji. Msisahau jambo hilo kamwe. Huu ndio wakati ambao, labda, huenda Mungu anafanya wito Wake wa mwisho. Sijui. Yeye atafanya wito Wake wa mwisho, siku moja. Lini? Sijui. Lakini ninawaambia, kulingana na ono hilo, inaonekana kama kwamba huyo Bibi-arusi anakaribia kukamilika.

Yaangalieni yale makanisa ya kawaida yakiingia. Wakati yule mwanamwali aliyelala alipokuja kutafuta Mafuta, alishindwa kuyapata. Bibi-arusi akaingia. Unyakuo ukapaa juu. "Walipoenda kununua Mafuta, Bwana-arusi akaja."

Je! Mmelala? Amkeni, upesi, na mjirudie. Na hebu tuombe, kila mmoja, kama kwamba tunakufa dakika hii, katika Jina la Bwana. Hebu, kila mmoja, na aombe kwa njia yako mwenyewe.

90 Mungu Mwenyezi, uturehemu. Bwana, unirehemu mimi. Turehemu sisi sote. Inatufaidia nini, haidhuru tunafanya nini, kama tukikosea katika mambo haya? Nasimama na kuomba rehema, Ewe Mungu, kabla mji huu mkuu haujazama chini ya bahari na hukumu za Mungu kuenea kwenye pwani hii. Naomba, Mungu, ya kwamba Wewe utamwita Bibi-arusi Wako. Nawakabidhi Kwako sasa, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

www.messagehub.info

Mahubiri Na

William Marrion Branham

"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7